SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**LAAC** yaitaka TAMISEMI iwawajibishe waliotumia vibaya fedha za h/shauri
UKURASA 3



**Lukaku, Werner nje mwezi mmoja**
UKURASA 23

Nipashe
Jumatatu Oktoba 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580744
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Ujenzi daraja la JPM wadaiwa kuhujumiwa

• **CCM** yasema madai hayo ya mradi huo wa bil. 700/- lazima yachunguzwe... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**ZAHANATI ILIVYOJENGWA KWA MIAKA 28 KIJIJINI**
ZAHANATI ya Kijiji cha Isowezy Kata ya Isansa wilayani Mbozi mkoani hapo...

UKURASA WA 5
**MTI WA MAAJABU SASA KUWA KIVUTIO UTALII**
HIFADHI ya Taifa ya Nyerere imeamua kuuacha mti wa ajabu wa asili uliokuwa...

UKURASA WA 18
**PINDA AWAONYESHA WASOMI FURSA KILIMO**
WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewataka wasomi kuchangamkia fursa...

## Diwani jela miezi 6 uharibifu wa mali

UKURASA 2



Rais wa Burundi, Evarist Ndayishimiye (wapili kulia), akitambulishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (kulia), kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakati alipowasili nchini kwa ziara ya kitaifa. Rais Ndayishimiye aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa kiwanda cha uzalishaji wa mbolea cha Itracom kinachojengwa kwa uwezeshaji wa Benki ya CRDB mkoani Dodoma. **PICHA: IKULU**

# Rais Ndayishimiye aipongeza CRDB kuimarisha uhusiano

UKURASA 2

**MICHEZO** **AZAM: CAF BASI, AKILI KWA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Diwani jela miezi 6 uharibifu wa mali

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro mkoani hapo, Lucas Lemomo, amehukumiwa jela miezi sita bila kulipa faini kwa kosa la uharibifu wa mali katika Mahakama ya Mwanzo Ngerengere, wilayani Morogoro.

Lemomo ambaye ni Diwani wa Kata ya Matuli, alishtakiwa kwa makosa matatu yote ya uharibifu wa mali kwa kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kuharibu mazao.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Ngerengere, Godfrey Ng'itu, alieleza juzi wakati akitoa hukumu kuwa Lemomo alikabiliwa na kesi namba 133 ya mwaka 2021 mahakamani hapo na mlalamikaji ni Athuman Abdallah, mkazi wa Mikobora, Kata ya Ngerengere na kesi ya pili namba 122 ya mwaka 2021, mlalamikaji ni Athuman Abdallah, mkazi wa Visaraka Ngerengere.

Hakimu wa mahakama hiyo alisema baada ya upande wa mshtaka kuthibitisha shtaka pasipo shaka lolote, mshtakiwa katika kesi zote mbili ametiwa hatiani kwa mujibu wa fungu 37(1) kanuni za Mwenendo wa Makosa ya Jinai katika Mahakama ya Mwanzo.

Hakimu Ng'itu alisema hukumu haikuwa na mbadala wa kulipa faini.

Mshtakiwa kwenye kesi ya kwanza amehukumiwa kwenda gerezani miezi sita na baada ya kutoka ametakiwa kulipa fidia ya mazao yaliyoharibiwa na mifugo Sh. 79,000.

Kesi ya pili amehukumiwa kwenda jela miezi sita bila faini na akitoka ametakiwa kulipa fidia ya Sh. 440,000 na kwamba kifungo hicho ni kwa pamoja wakati kesi yake nyingine ya jinai itasomwa hukumu Novemba 3, 2021.

# Ujenzi daraja la JPM wadaiwa kuhujumiwa

**Na Richard Makore,** MWANZA

MADAI kuhusu kuhujumiwa kwa daraja la JPM linalojengwa eneo la Kigongo-Busisi, mkoani hapo kwa gharama ya Sh. bilioni 700 yameibuliwa katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika mwishoni mwa wiki jijini Mwanza, Katibu Mwenezi wa CCM katika Wilaya ya Ilemela, Denis Nyamlekela alisema, Oktoba 14, mwaka huu, walipata taarifa mbaya kutoka kwa mmoja wa mafundi wa mradi huo kwamba vipimo vya bomba na nondo zilizokubaliwa katika mkataba vimechakachuliwa.

Alisema mtoa taarifa huyo ambaye mpaka sasa anafanya kazi katika mradi huo, alisema vipimo vya mabomba na nondo zilizokubaliwa katika mkataba wa ujenzi uliosainiwa vimechakachuliwa.

Nyamlekela alisema Oktoba 14, mwaka huu yeye na kamati ya siasa wakitokea wilayani Chato walipata taarifa hiyo na kwamba vipimo vya mabomba yanayoshuka chini majini vimechakachuliwa na kwamba kuna hatari ya daraja hilo kutokuwa imara.

Mjumbe huyo wa kikao hicho alisema, kuna haja ya kufanya uchunguzi kuhusu taarifa hiyo ili kujiridhisha ukweli wake.

Aliongeza kuwa mradi huo ni muhimu kwa uchumi wa nchi na umegharimu fedha nyingi ni lazima tahadhari zote zichukuliwe ili kuulinda. Daraja hilo ambalo linajengwa na kampuni kutoka nchini China, linaunganisha wilaya za Misungwi na Sengerema.

Akizungumzia madai hayo, Mwenyekiti wa chama hicho mkoani Mwanza, Antony Diallo, alisema kuna haja ya kufanya uchunguzi kuhusu suala hilo.

Hata hivyo, Diallo alionyesha wasiwasi wake kuhusu ukweli wa taarifa hizo kwa madai kuwa mradi huo unasimamiwa na wataalamu walioaminiwa na serikali.

"Mimi siamini taarifa hizi kwamba vipimo vya bomba na nondo vilivyokubaliwa kitaalamu katika mkataba kwa sasa havifuatwi, ila uchunguzi ufanyike," alisema Diallo ambaye alisimamia kikao hicho.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alipouliza kuhusu madai hayo alisema, haamini kama ni kweli.

Alisema hawezi kuamini taarifa za barabarani, lakini alisema uchunguzi utafanyika ili kujiridhisha kuhusu madai yaliyotolewa. Aliongeza kuwa kuna wataalamu wa kutosha walioaminiwa kusimamia mradi huo mkubwa na kimkakati mkoani mwake.

Kikao hicho ambacho pia kilihusisha watendaji, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Wilaya, Kamati ya Usalama ya Mkoa na Watendaji wa serikali mkoani Mwanza kilikuwa kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025.



Meneja Mwandamizi wa Idara ya Biashara wa Benki ya NMB, Christopher Mgani, akielezea faida inayopatikana na mikopo ya Mining Club kwa ajili ya wachimbaji wakubwa na wadogo kwenye semina iliyoandaliwa na benki hiyo. Benki ya NMB imeanzisha Mining Club ikilenga kuwakwamua wadau wa madini kifedha na kuwasaidia kufanya shughuli zao kisasa zaidi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Ndayishimiye aipongeza CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imepongezwa kwa kufanikisha kuimarika kwa ushirikiano wa kibiashara kati ya Tanzania na Burundi kupitia huduma zake za kibenki.

Akizungumza jijini Dodoma mwishoni mwa wiki baada ya kuweka jiwe la msingi la uijenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizers Limited cha wawekezaji kutoka Burundi, Rais Evariste Ndayishimiye alisema, Benki ya CRDB imekuwa mshirika mkubwa wa kuimarisha biashara na uwekezaji baina ya nchi hizo mbili. Benki ya CRDB imetoa mkopo wa kuwezesha ujenzi wa kiwanda hicho cha mbolea.

"Uwezeshaji uliofanywa na benki katika ujenzi wa kiwanda hiki cha mbolea ni ushahidi tosha wa namna gani benki imejikita katika kufanikisha kuimarika kwa biashara na uwekezaji baina ya nchi zetu zenye udugu wa karibu," Rais Ndayishimiye alisema.

Alisema uwekezaji huo wa raia kutoka nchini kwake, utawezesha kiwanda cha mbolea cha Itracom kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka na kutoa ajira kwa Watanzania wasiopungua 10,000.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema benki yake yenye matawi matatu nchini Burundi imekuwa ikitoa mikopo kwa miradi mbalimbali ya kimkakati ya serikali ya Burundi na Tanzania. Benki inatarajia kufungua tawi la nne wilayani Gitega mwaka huu.

Nsekela alisema benki yake inafanya biashara kwa muda mrefu na wawekezaji wa Itracom huko Burundi kwa kuwapatia huduma zote za kibenki. Miongoni mwa miradi ambayo benki imefadhili Burundi ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha Fomi na kiwanda cha saruji huko Rutana ambacho benki imetoa mkopo wa Dola za Marekani milioni 10.

"Mheshimiwa Rais, uwapo wako hapa leo kuweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha Itracom ni ushahidi tosha wa kuimarika kwa uhusiano baina ya Burundi na Tanzania. Kama benki ya kizalendo yenye mtazamo wa kimataifa,

Benki ya CRDB ina mkakati wa makusudi wa kuwezesha kuimarika kwa uhusiano ya kibiashara na uwekezaji baina ya nchi za Afrika ya Mashariki ili kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu," alisema.

Kadhalika, alisema benki hiyo imeshawekeza mtaji wa Dola milioni 107 nchini Burundi katika sekta mbalimbali za uchumi wa nchi hiyo ukiwamo mradi wa kuzalisha umeme wa maji Mpanda.

Benki hiyo pia imewezesha kampuni ya Itracom kuwekeza katika kiwanda cha mbolea cha Minjingu kilichoko Babati mkoani Manyara. "Hapa nchini Tanzania benki yetu imewezesha kampuni ya Itracom kwa kuipatia mkopo wa dola 12 milion kwaajili ya ujenzi wa kiwanda cha Minjingu kilichopo Babati," Nsekela alisema.

Tangu ianzishe kampuni tanzu nchini Burundi mwaka 2011, Benki ya CRDB imetoa mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa kupitia kutoa ajira kwa Warundi na pia kulipa kodi mbalimbali za serikali kufanikisha maendeleo.

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara (MTUWASA), Mhandisi Rejea Ng'odya, akifafanua jambo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dastun Kyobya (kushoto) wakati ujumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya, ilipotembelea vyanzo vya maji vya MTUWASA. **PICHA: ABDALLAH KHAMIS**

# TAMISEMI yatakiwa kuwawajibisha wanaotumia vibaya fedha h/shauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeagizwa kuwachukulia hatua za kisheria watendaji waliotajwa kuhusika na matumizi mabaya ya fedha kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (LAAC), kufuatia ripoti ya ukaguzi maalum ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliyofanywa kwenye halmashauri hiyo mwaka 2018.

Akizungumza na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Grace Tendega, alisema kamati iliomba kufanyika ukaguzi maalum baada ya kukutana na matumizi ya fedha ambayo hayakufuata utaratibu.

"Tuligundua ukaguzi kama huu ulishafanyika mwaka 2018 na ripoti yake kukabidhiwa kwa TAMISEMI kwa ajili ya utekelezaji na kamati jana (mwishoni mwa wiki) ilipitia kuangalia kilichojiri," alisema.

Alisema katika kupitia ripoti hiyo walibaini kuwa CAG alitoa mapendekezo ambayo hayajatekelezwa na waliagiza TAMISEMI kutekeleza maagizo hayo na kuhakikisha kuwa watendaji ambao wametajwa kwa majina wanachukuliwa hatua.

Pamoja na kuwachukulia hatua watendaji, alisema kamati hiyo, iliomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ifanye kazi yake kwa kuwapeleka makandarasi kwenye bodi yao ili wawachukulie hatua kulingana na makosa waliyoyafanya.

Tendega alitaja baadhi ya mambo yaliyokwenda kinyume na taratibu ni ufungaji wa vitabu vya fedha, ujenzi wa machinjio isiyoisha na miradi mingine mingi.

Hata hivyo, alisema katika ukaguzi wao wa hesabu za mwaka wa fedha 2019/20, kamati imekutana na hoja hizo ambazo tayari zilishafanyiwa ukaguzi maalum.

"Kamati imeona kwa kuwa ilishafanyika, tusitumie fedha vibaya, tumeagiza maagizo hayo yatekelezwe," alisema.

Kuhusu kiasi cha fedha kilichotumika kinyume, Makamu Mwenyekiti wa LAAC, Selemani Zedi, alisema hawajapewa kwa ujumla kiwango na kwamba uchambuzi unaofanywa na TAMISEMI bado unaendelea.

"Bado ripoti inachambuliwa na TAMISEMI kubaini nani alihusika? Kwa lipi na linatokana na nini? Polisi, TAKUKURU zichukue hatua za kisheria. Wakandarasi na wahandisi nao wapelekwe katika bodi zao," alisema.

Katika hatua nyingine, LAAC imebaini dosari kadhaa kwenye Halmashauri za Mbogwe na Nyang'wale ikiwamo kutopeleka kikamilifu asilimia 10 ya mfuko wa wanawake, vijana na wenye ulemavu na asilimia 40 ya mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo.

Zedi alisema kamati imebaini kutopelekwa katika kata na vijiji kwa asilimia 20 ya fedha zinazotolewa na serikali kama fidia ya mapato ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa.

"Dosari nyingine ni usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ambao wamebaini katika halmashauri nyingi kuwa na upungufu, kwa mfano wa halmashauri ilikuwa ikusanye Sh. milioni 400, lakini zilizokabidhiwa ni Sh. milioni 200," alisema.

Kadhalika, alisema usimamizi wa miradi ya maendeleo bado ni tatizo na wamekuta halmashauri zina miradi mingi, lakini haijakamilika.

"Mfano Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ambayo ina miradi 75 ipo katika hatua za misingi, lenta na walipoulizwa walijibu kuwa wananchi walihamasishwa kuchangia ujenzi wa zahanati na vituo vya afya na kwamba serikali itakuja kumalizia, lakini haikufika kwenda kumalizia," alisema.

## WFP ilivyopata soko la mtama

**Na Faustine Feliciane,** DODOMA

ZAIDI ya wakulima 22, 000 wa wilaya tano za mkoa wa Dodoma, wameunganishwa kwa wanunuzi wa mtama Sudan Kusini ambapo soko la zao hilo ni kubwa.

Wakulima hao wameunganishwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ambapo wameshauza jumla ya tani 17,000 ya zao hilo ambapo zimewaingizia zaidi ya shilingi bilioni 9 kwa miaka miwili pekee.

Akizungumza jijini hapa na waandishi wa habari, Mkuu wa ofisi ndogo ya WFP, Neema Nima Sitta, alisema wakulima ambao wameanza kunufaika na kilimo hicho ni kutoka wilaya za Dodoma, Kondoa, Chemba, Mpwapwa, Bahi na Dodoma.

Alisema wakulima hao wamenufaika na mradi wa WFP wa kilimo himilivu cha mtama unaoendeshwa kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

"Zao la mtama limekuwa na soko kubwa Sudan Kusini na WFP inaendesha programu maalum ya kulima zao hilo katika vijiji zaidi ya 200 kwenye wilaya za mkoa wa Dodoma," alisema Nima.

Alisema WFP linawatafutia soko wakulima hao kwa mashirika binafsi katika nchi hiyo, pia shirika hilo likiwa sehemu ya wanunuzi kwa ajili ya kambi za wakimbizi.

"Katika mradi huo ambao tunashirikiana na serikali, tumeanza na vijiji 203 katika mkoa wa Dodoma na lengo ni kupanua mradi huu kwani kuna mahitaji makubwa ya mtama Sudan kusini," alisema.

Hata hivyo, alisema mtama huo unaopata soko nchini humo unalimwa kwa mfumo wa kilimo hai (organic), hivyo pia kuondoa matumizi ya mbolea za viwandani na dawa," alisema.

"Sisi WFP tukiwa pia kama patna wa serikali tunajivunia mradi huu, umekuwa na mafanikio makubwa, lakini tumegundua zao hili limekuwa hitaji kubwa kwa nchi ya Sudan Kusini," alisema Nima.

Aidha, alisema kutokana na uhitaji huo mkubwa kwenye soko, WFP wanafikiria kupanua mradi huo na kufikisha kwenye wilaya nyingi na mikoa mingine Tanzania.

# Wastaafu wafuatilia nauli miaka minne

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya wastaafu Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, wamelalamikia kitendo cha halmashauri hiyo kutowalipa nauli ya kurudi kwao tangu walipostaafu miaka minne iliyopita hali inayosababisha waishi maisha ya shida huku wakisubiria malipo hayo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana kwa niaba ya wastaafu hao, Milson Sanga ambaye ni mwenyekiti wao, alisema wapo 18 hawajalipwa stahiki zao ambazo ni mapunjo ya kiinua mgongo (pensheni) pamoja na fedha kwa ajili ya nauli baada ya kustaafu mwaka 2018.

Alisema wamejitahidi kufuatilia fedha hizo kwa muda mrefu, lakini kila wanapofika kuuona uongozi wa halmashauri hiyo wanaambiwa wasubiri watalipwa huku miaka inakwenda bila mafanikio, hali inayowafanya waishi kwa shida kwa kuwa wanaishi nyumba za kupanga.

"Hivi unavyotuona tumeathirika kisaikolojia, ni kama tumetelekezwa, kiinua mgongo chenyewe tumelipwa pungufu kwa kuwa kilikokotolewa kwa daraja la zamani ambalo ni TGTSE, wakati tunastaafu tulikuwa tumepandishwa daraja jingine na kuwa TGTSF, nauli hatupewi, tunajiuliza tumeitumikia serikali kwa uaminifu mkubwa... malipo yake ndiyo haya kwetu?"... alihoji.

Alisema kuwa kibaya zaidi halmashauri hiyo bado haijawasilisha kiwango kipya ambacho ni ongezeko la michango yake kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) ambayo iliongezeka baada ya badiliko la mshahara miaka minne iliyopita hali iliyochangiwa na mfuko huo kuchelewa kuwalipa mapunjo yao ya kiinua mgongo fedha ambazo ni haki yao.

"Hii ipo katika barua yenye kumb Na. PSSSF/RUK.AC.56/84/01/165 ya Machi 16, 2021 ambayo meneja wa mfuko huo alimwandikia barua mkurugenzi wa halmashauri akimpa siku 30 ili awasilishe michango hiyo, ili PSSSF ishughulikie madai ya wastaafu tisa, lakini mpaka leo hii mkurugenzi hajawasilisha michango hiyo, jamani tunateseka kwa sababu ya stahiki zetu hii ni halali kweli," alihoji.


**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI.......152 LA 2021**
**MAMY SELEMANI MLINDWA...........MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EMMANUEL PETER...MDAIWA**
**WITO WA KUITWA SHAURINI**
**EMMANUEL PETER POPOTE ULIPO**

MAMY S. MLINDWA amefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na nyumba lililopo kinondoni (mwananyamala) shauri husika limepangwa kusikilizwa/kutajwa tarehe 25-10-2021 saa 3:00 asubuhi mbele ya mh R.Mbilinyi. hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa baraza hili leo tarehe 15 mwezi 09....2021

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI**

116529102

# Zahanati ilivyojengwa kwa miaka 28 kijijini

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SONGWE

ZAHANATI ya Kijiji cha Isowezy Kata ya Isansa wilayani Mbozi mkoani hapo, ambayo ilikuwa kila inapojengwa kwa zaidi ya miaka 20 inabomoka katika mazingira ya kutatanisha kutokana na imani za kishirikina, hatimaye ujenzi wake umekamilika.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omari Mgumba, alitembelea zahanati hiyo na kuizindua alielezwa kuwa ujenzi wake umekamilika hivi karibuni na inatarajiia kuanza kutoa huduma.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Rehema Simbeye, alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa zahanati hiyo ilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi tangu mwaka 1993. Simbeye alisema kuwa hadi kukamilika kwa ujenzi wa zahanati hiyo, gharama iliyotumika ni shilingi 69,246,000.

Aliongeza kuwa, nguvu ya wananchi iliyotumika ni sawa na shilingi 16,446,000 na serikali kuu ikitoa shilingi milioni 50, huku wadau wengine wakichangia vifaa mbalimbali.

Kando ya mkutano huo, gazeti hili lilitaka kujua nini kilichosababisha ujenzi huo kusuasua kwa miaka hiyo, ambapo baadhi ya wananchi walisema ni imani za kishirikina.

Mmoja wa wananchi hao, Enea Mwashinga, alisema kuwa ujenzi wa zahanati hiyo ulikuwa ukikwama kwa muda wote huo kutokana na kubomoka zaidi ya mara tatu katika mazingira ya kutatanisha wakati shughuli za ujenzi zikiendelea kutokana na mambo ya kishirikina. "Kuna wakati unaweza kuamini kuwa ushirikina upo, maana zaidi ya mara tatu zahanati ilikuwa ikibomoka katikati ya shughuli za ujenzi, hali ambayo ilisababisha wananchi kususa kwa muda," alifafanua Mwashinga.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa Mgumba baada ya kuizindua zahanati hiyo alimtambulisha mganga wa zahanati hiyo, na kuwaomba wananchi wampatie ushirikiano ili asije akakimbia.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipokea zawadi kutoka kwa Kiongozi Mkuu wa Kanisa la Greek Orthodox, Baba Mtakatifu Beatitude Theodoros, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Dk. Mpango akutana na kiongozi Greek Orthodox

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango jana alikutana na kufanya mazungumzo na Kiongozi Mkuu wa Kanisa la Greek Orthodox, Baba Mtakatifu Beatitude Theodoros II, Ikulu Dar es Salaam.

Makamu wa Rais alisema Tanzania imefurahishwa na ujio wa kiongozi huyo na kumwomba kuendelea kuiweka Tanzania katika maombi yake ya kila siku.

Alisema tangu uhuru Tanzania imekuwa kitovu cha amani na kuendelea kuheshimu umuhimu wa dini zote kupitia ibara ya 19 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, alisema viongozi wa dini nchini wamekuwa ndiyo msingi wa amani iliopo.

Alisema serikali inatambua mchango unaotolewa na taasisi za dini nchini kwa kushiriki vema kuleta maendeleo hususan katika sekta za elimu na afya hasa katika maeneo ya pembezoni ya nchi.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, mchango wa Kanisa la Orthodox nchini ambao ni pamoja na ujenzi kliniki 90 pamoja na hospitali katika mkoa wa Kagera na shule katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Aidha, alisema Tanzania itaendelea kushirikiana kwa karibu na Kanisa la Orthodox nchini pamoja na dini zingine katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa upande wake Kiongozi Mkuu wa Kanisa la Greek Orthodox, alisema amefurahishwa kushiriki mazungumzo na Makamu wa Rais, na kumwomba kufikisha salamu zake kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amemtaja kama mfano wa upendo unaopatikana Tanzania.

Alisema Tanzania ni nchi imara sana ambayo amekuwa akiitaja katika maeneo mbalimbali duniani ikiwamo alipofanya ziara nchini Russia na kukutana na Rais wa nchi hiyo, Vladmir Puttin, alipoulizwa juu ya nchi imara barani Afrika aliitaja Misri ikifuatiwa na Tanzania.

# Utafiti kumaliza tatizo la tembo kuvamia mashamba

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

KUTOKANA na kukithiri vitendo vya tembo kuvamia makazi ya watu na kula mazao ya wakulima katika mashamba, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi imeamua kufanya utafiti ili kumaliza tatizo hilo.

Utafiti huo unafanywa na Mikumi kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) ili kubaini sababu kubwa za wanyama hao kwenda maeneo ya wananchi na kufanya uharibifu huo.

Akiongea na waandishi wa habari, waliotembelea Hifadhi ya Mikumi, Kamshina Msaidizi wa Uhifadhi, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi (TANAPA), Mathew Mombo, alisema utafiti huo umeshaanza kufanyika pembezoni mwa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo.

Alisema utafiti huo umelenga kujua tabia za wanyama hao na kuwafunga vifaa maalumu kwa ajili ya kuwafuatilia kwa karibu ili kama wapo nje ya hifadhi waweze kurudishwa mara moja.

Alisema lengo la utafiti huo ni kulenga kusaidia kupunguza tatizo la wanyama hao kwenda katika maeneo ya wananchi kwa kuwashambulia na kufanya uharibifu wa mazao na miundombinu.

Mombo alisema moja ya matokeo chanya ya utafiti huo ni kusaidia kupunguza changamoto mbalimbali zinazotokana na tembo dhidi ya wananchi wa vijiji vya pembezoni ili pia yaweze kutumika katika maeneo mengine yenye usumbufu wa wanyama wanaofanya uharibifu.

Mkuu huyo ya Hifadhi ya Mikumi, alisema wakati wakiendelea na utafiti huo, wameshaunda kikosi maalumu cha kufuatilia wanyama hao wanaokwenda kwa wenyeji ambacho kinafanya kazi saa 24 ili kuwarudisha ndani.

"Wanyama wote wanaotoka ndani ya hifadhi yetu na kwenda kwenye vijiji kufanya uharibifu wowote, hifadhi yetu inachukulia kwa uzito mkubwa ili kupunguza athari zake katika jamii na tumeunda timu maalumu ya kufanya kazi hiyo kwa muda wa saa 24," alisema Mombo.

Alisema wametoa mawasiliano kwa viongozi wa vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi hiyo ili kutoa taarifa mara moja na wao kwenda kuwadhibiti wanyama hao bila kuleta uharibifu wa aina yoyote.

Kwa upande wake Mkuu wa Kituo cha Wanyamapori Kingupira, Samuel Mtoka, kutoka TAWIRI, alisema utafiti huo unaofanywa endapo utakamilika kwa wakati utasaidia kwa kiasi kikubwa kumaliza tatizo hilo la wanyama kuvamia katika makazi ya watu.

Alishauri wakati utafiti huo ukiendelea wakulima kupanda mimea ya pilipili pembezoni mwa mashamba yao, kufuga nyuki na kutumia moshi unaotokana na kinyesi cha wanyama kwa kuwa tembo hawapendi.

HABARI KITAIFA

## Wataka kutambuliwa siku ya watu maskini

**Na Salome Kitomari**

MWANAHARAKATI wa watu maskini, Venance Magombera, ameitaka serikali na wananchi kuitambua na kuisherehekea siku ya watu wanaoshi kwenye umaskini uliopindukia.

Hatua hiyo ni sehemu ya kuwafariji na kuunganisha nguvu za namna ya kuwakomboa kiuchumi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Magombera, ambaye ni kiongozi wa Taasisi ya Organized by all together in Dignity (ATD), alisema kutokana na shughuli za kuwainua maskini wamefanikiwa kuunda vikundi vya wanawake ambao wanafanya ujasiriamali unaowakomboa kwenye hali duni.

Alisema wanatarajia kuwa na maonyesho ya bidhaa zinazotengenezwa na watu wa hali duni yatakayofanyika Jumapili eneo la Alliance Francaise, ikiwa ni maadhimisho ya siku ya kimataifa ya kupunguza umaskini, ambayo kwa Tanzania huadhimishwa Oktoba 17 kama siku ya watu fukara.

Vikundi hivyo ni wanawake wanaopinga umaskini cha Ilo-ganzara (IWAPOA) na wanawake wajasiriamali wa Tandale, Boko na Tegeta (TABOTE), ambao wanajishughulisha na kugonga kokoto kupata kipato na sasa wanafanya ujasiriamali wa kutengeneza sabuni mbalimbali ili kujipatia kipato kwa ufadhili wa Ubalozi wa Ufaransa nchini.

"Kila siku tunasikia siku ya jambo fulani, kila Oktoba 17 ni siku ya watu maskini lakini hakuna anayeipa kipaumbele, umaskini ni mgumu sana mnavyotuona hapa tunatwanga kokoto usiku na mchana kuweza kutoka kwenye hiyo hali kwa kufanya ujasiriamali ni hatua kubwa sana, tunashukuru Ufaransa kwa kuendelea kutuwezesha miradi midogo midogo ya kuwainua watu wa hali duni," alisema Magombera.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa kinamama wa kijiji cha Swagaswaga Wilaya ya Kondoa, ikiwa ni mwendelezo wa kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani iliyofanyika juzi **PICHA PETER MKWAVILA**

# Mti wa maajabu waachwa kuwa kivutio cha utalii

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HIFADHI ya Taifa ya Nyerere imeamua kuuacha mti wa ajabu wa asili uliokuwa ukitumiwa kufanya matambiko na jamii kwa ajili ya utatuzi wa masuala mbalimbali ili kuwa sehemu ya kivutio cha wageni wanaotembelea hifadhi hiyo.

Mti huo unafahamika kama Marula umekuwa kivutio kutokana na kuota katikati ya barabara kuu na kushindwa kung'olewa wakati wa upanuzi ndani ya hifadhi hiyo hali iliyosababisha kuwekwa barabara pacha.

Barabara hiyo inatokea Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani.

Akizungumzia mti huo, Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (TANAPA), Seth Mihayo, alisema mti huo umekuwa kivutio kwa sababu wakati wa upanuzi wa barabara licha ya kutumia vifaa vya kisasa kama magreda ya kukata miti mikubwa, mti huo ulishindikana kukatika na badala yake vifaa hivyo viliharibika na mti huo kuendelea kubaki.

Alisema baada ya kufanyika utafiti historia inaonyesha kulikuwa na vijiji kipindi cha nyuma ndani ya hifadhi hiyo ikiwamo kijiji cha Mloka ambavyo wazee wa miaka ya nyuma walikuwa wakifanya mambo ya mizimu na matambiko mbalimbali ndiyo maana wameamua kuuenzi uwe sehemu ya kivutio cha utalii.

Mihayo, alisema kivutio kingine ni kuwapo kwa maeneo waliokuwa wakiishi mijusi mikubwa miaka ya nyuma ambayo kwa sasa mabaki na mifupa yake ilipelekwa Berlin nchini Ujerumani kwa ajili ya kuhifadhiwa na makazi halisi ya mijusi hiyo ilikuwa ndani ya hifadhi hiyo ya Nyerere.

Alisema kumekuwa na vivutio na maeneo ya kihistoria ambayo ni pamoja na kumbukumbu ya vita vya majimaji ambapo Mtemi Kinjekitile Ngwale alichukua maji kwenye moja ya mito iliyopo hifadhini hapo kuaminisha jamii aliyokuwa akiongoza kuwa yanauwezo wa kuzifanya risasi kuwa maji. Mmoja wa wazee wa eneo hilo kutoka katika Kijiji cha Mloka jirani na hifadhi hiyo, Mohamed Haule akizungumzia maajabu ya mti huo alisema umekuwa ukisababisha baadhi ya watu wanaofika katika maeneo hayo kufanya shughuli tofauti za matambiko. Akizungumzia kuhusu kushindwa kutolewa kwa mti huo wakati wa upanuzi wa barabara, alisema yeye binafsi alishuhudia magreda hayo yalivyoshindwa kung'oa mti huo na kuishia kuharibika.

Akizungumza na waandishi wa habari, kwenye lango kuu la Mtemele la kuingia katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, mmoja wa watalii wa ndani Mratibu wa Umoja wenye magari ya Landrover, Meja Mbuya, alisema amelazimika kufika katika hifadhi hiyo kwa ajili ya kujionea mti huo wenye maajabu.

Mbuya alisema katika kumuenzi Hayati Nyerere kwa vitendo, wameamua kuhamasisha utalii wa ndani kutembea hifadhi mbalimbali na kwa kuanzia walianza na Hifadhi ya Mikumi na sasa wanaendelea na Hifadhi ya Nyerere ambayo ni kubwa kwa bara la Afrika.

# PM asisitiza umuhimu mifumo usalama mijini kupitia TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imetenga shilingi bilioni 170 kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa katika mwaka wa fedha 2021/2022, huku akisisitiza umuhimu wa mifumo ya usalama kupitia TEHAMA katika miji mbalimbali nchini.

Majaliwa ameyasema mwishoni mwa wiki alipofungua Mkutano wa Tano wa Mwaka wa TEHAMA Tanzania uliofanyika jijini Arusha.

Kuhusu Mkongo wa Taifa, fedha hizo zitawezesha kujenga kilomita 4,244 za mkongo huo ili kufikisha jumla ya kilomita 12,563.

"Lengo letu ni kuwawezesha watoa huduma za mawasiliano kutumia miundombinu hii kuboresha huduma za mawasiliano nchini na kurahisisha ufikishwaji wa intaneti kwenye ofisi mbalimbali za sekta ya umma na binafsi," alisema.

Majaliwa aliagiza Wizara ya Habari, Sayansi na Teknolojia ya Habari isimamie kwa karibu mradi wa upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili wananchi wengi zaidi washiriki katika ujenzi wa uchumi wa kidijitali.

"Hivi sasa serikali imejenga kilomita 8,319 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi Septemba 2021. Malengo yetu kama serikali ni kujenga hadi kilomita 15,000 ifikapo mwaka 2024/2025. Hili linahitaji uwekezaji mkubwa na serikali imejipanga kuwekeza vilivyo, lakini tunakaribisha wabia na wawekezaji katika eneo hili pamoja na maeneo mengine ya TEHAMA," alisema.

Kuhusu umuhimu wa uwapo wa mifumo ya usalama kupitia TEHAMA katika miji mbalimbali nchini, alisema zitasaidia kuongeza usalama kwa kuwa utawezesha kuwa na rekodi za matukio mbalimbali yakiwamo yakihalifu katika maeneo hayo. "Nilipata nafasi ya kufanya ziara China na nikatembelea ilipo kampuni ya Huawei, hapo nilijionea teknolojia kubwa na za kisasa ambazo tunaweza kuzitumia hapa nchini pia," alisema Waziri Mkuu.

Baada ya kufungua mkutano huo, Majaliwa pia alizindua mwongozo wa usajili wa wataalamu wa TEHAMA na kutoa vyeti kwa baadhi ya wataalamu wa TEHAMA ambao wamesajiliwa. Waziri wa Habari, Sayansi na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, alisema wizara yake imejipanga kujenga kituo mahiri cha kukuza utaalamu na utafiti nchini ambacho kitajengwa jijini Dodoma kwa kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali "Digital Tanzania."

Miongoni mwa waliotunukiwa tuzo ni pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kulibeba suala la TEHAMA kwa nguvu zake zote na kuliweka kwenye vipaumbele vya serikali. Awali, katika mahojiano yake na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huawei Tanzania, Damon Zhang, alisema kampuni hiyo ipo tayari na imejitolea kufanya kazi na serikali katika kuleta maono ya pamoja ya kukuza uchumi wa kidijiti, sambamba na kudhibiti changamoto zilizoletwa na ustawi wa TEHAMA.

"Tunajitolea kuendelea kukuza ujumuishaji wa kidijiti kwa kila mtu, kila nyumba, na kila shirika kwa ajili ya kuandaa Tanzania iliyounganishwa," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TFF sasa itathmini wawakilishi wetu CAF kabla ya kupewa jukumu hilo

**PAMOJA** na juhudi kubwa iliyofanywa na klabu ya Simba msimu uliopita kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika hadi kuiongezea Tanzania pointi na hivyo kufikia kiwango cha kuingiza timu nne, sasa tunaendelea kuitegemea timu hiyo pekee kwenye Kombe la Shirikisho Afrika kulibeba tena taifa.

Tanzania ilikuwa miongoni mwa timu 12 zilizofikisha pointi za kuruhusiwa kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika kwa msimu huu wa 2021/22. Hata hivyo, tayari timu tatu zimetolewa na imebaki Simba pekee ambayo imeangukia Kombe la Shirikisho Afrika baada ya jana kutolewa na Janweng Galaxy ya Botwana kwenye Ligi ya Mabingwa, huku Yanga ambayo nayo ilikuwa katika michuano hiyo, ikitolewa raundi ya awali na Rivers United ya Nigeria baada ya kipigo cha bao 1-0 nyumbani na ugenini.

Kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC imetolewa na Pyramids FC ya Misri raundi ya kwanza kwa kufungwa bao 1-0 ugenini juzi baada ya mchezo wa awali timu hizo kutoka suluhu Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Wawakilishi wengine kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Biashara United, wenyewe ni wazi kama ni kushindwa kuendelea katika michuano hiyo, basi kumechangiwa na mambo mengi, lakini kubwa likionekana ni kiuchumi.

Hiyo ni kutokana na ushindi wa mabao 2-0 walioupata nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya, kushindwa kwenda ugenini kuulinda katika mechi ya marudiano kwa sababu ambazo kama ingekuwa imejipanga ama kujizatiti vema kiuchumi, hilo lisingetokea.

Ikumbukwe pia Biashara ilisafiri kwenda Djibouti kuivaa FC Dikhil katika hatua ya awali ya michuano hiyo, ambapo ilifika siku ya mchezo wa kuelekea moja kwa moja uwanjani kucheza mechi hiyo na kushinda, jambo ambalo pengine viongozi wa timu hiyo waliona hata kwa safari ya Libya linawezekana.

Pamoja na viongozi wa Biashara United, kueleza kwamba awali walipata ndege ya kukodi kabla ya kuahirisha safari zake kutokana na kuhofia hali ya usalama na kisha kupata Air Tanzania kwa ushirikiano na Shirikisho la Soka nchini (TFF), lakini hilo lilifanyika wakati muda umeshawatupa mkono, hivyo kushindwa kupata vibali vya anga kutoka Sudan, Sudan Kusini na Libya kwa kile kilichoelezwa kutokufanya kazi siku ya Ijumaa na Jumamosi.

Kwa hili Biashara United inapaswa kubeba lawama zote yenyewe kwa kuliaibisha taifa kwani ni wazi ilikuwa inafahamu kuwapo kwa safari ya Libya, hivyo ilipaswa kujipanga mapema kama ambavyo wapinzani wao walivyomudu kufika nchini siku nne kabla ya mchezo wao na kufanikiwa kurejea kwao wakitumia anga hilo hilo walilokosa vibali.

Kwa sasa Biashara inasubiri tu huruma ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya kutuma maombi ya changamoto ya usafiri na kuomba mchezo huo usogezwe mbele hadi Jumatano wiki hii, lakini wakati wakisubiri huruma hiyo, wapinzani wao waliingiza timu uwanjani na taratibu zote za kupewa ushindi kufanyika.

Kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Simba kupigania nafasi hizo nne, sisi tunaona ipo haja sasa kwa TFF kuanzia msimu ujao kuhitaji kujiridhisha kwa kupata tathmini na hali nzima ya kiuchumi kwa kila klabu inayopata nafasi ya kuiwakilisha nchi kimataifa kabla ya kukabidhiwa jukumu hilo rasmi.

Lakini klabu zinazopata nafasi hizi za kuiwakilisha nchi kimataifa, kujitadhimini zenyewe ndani na nje kiuchumi na hata uwezo wao dimbani kabla ya kukubali jukumu hilo na kama zinaona ni mzigo kwao, kukubali kutoa nafasi hiyo kwa klabu zenye uwezo ili kutolitia taifa katika aibu kama hii tena.

Lengo letu ni kuona nafasi hizi nne tulizozipata kimataifa, zinaendelea kulindwa kwa kupeleka timu zenye uwezo uwanjani na hata kiuchumi ili kulifanya soka letu liwe katika kiwango cha juu barani Afrika na si kuendelea kuitegemea klabu moja tu kila msimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Biashara United sasa iwe funzo kwa wawekezaji kuheshimiwa

**LICHA** ya kushinda mabao 2-0 nyumbani, wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wameshindwa kwenda ugenini nchini Libya kucheza mechi ya marudiano.

Ilianza kama minong'ono au tetesi kuwa Biashara United hawana pesa za kusafiri kwenda nchini Libya kwenye mechi ya marudiano. Lakini wenyewe viongozi wa timu hiyo walikuwa wakikataa na kusema kuwa kila kitu kinakwenda vizuri na wanafanya maandalizi ya safari. Hata hivyo, kila siku za kuondoka zilivyozidi kukaribia, ilionekana hakuna dalili yoyote ya safari. Hakuna kiongozi yeyote wa Biashara United aliyejitokeza kwenye vyombo vya habari na kukiri waziwazi kuwa hali ni mbaya na kuomba msaada ili waondoke.

Lisemwalo lipo na kama halipo linakuja. Hali hii ikimsukuma Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, kuliambia Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhakikisha kuwa timu hiyo inapatiwa msaada wa hali na mali, kuhakikisha inasafiri.

TFF ikatekeleza maagizo hayo, lakini kwa sababu ya kuchelewa pakaibuka changamoto nyingine. Mara nyingi hata ukichelewa safari na ukapanda daladala ukitegemea itafika kwenye muda uliopangwa, ndiyo siku hiyo unakuta inakamatwa na askari wa usalama barabarani, inaharibika njiani, au inapitia kituo cha mafuta kuweka mafuta. Ili mradi tu uchelewe zaidi na hii inatufunza kuwa na tabia ya kuwahi sehemu yoyote ile unayotaka kwenda au kwenye miahadi na mtu.

Usafiri ukapatikana, lakini ikaja changamoto ya upatikanaji vibali vya anga kutoka kwenye nchi za Sudan, Sudan Kusini na Libya na hii inatokana na nchi hizo kutofanya kazi siku za Ijumaa na Jumamosi.

Sasa hilo lipo nje ya uwezo wa serikali na TFF pia. Chochote kitakachotokea hapa wakulaumiwa ni Biashara United wenyewe. Kama wangesema mapema, serikali, TFF na wadau wangeianza kazi hiyo mapema na wangeondoka nchini kabla ya Ijumaa na Jumamosi. Sidhani kama hapa unaweza kuilaumu serikali au TFF. Hivi vitu vinatakiwa vifanywe mapema sana.

Kwa sasa tunasubiria tamko kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF) juu ya mechi hiyo iliyopita. Wakati tunasubiria hilo, kuna jambo la kujifunza hapa kwa wadau wote wa soka, kuanzia viongozi, waandishi wa habari, wachambuzi, wanachama, mashabiki na wapenzi wa soka nchini Tanzania.

Ni kwamba tukiona timu imepaa na kusafiri kwenda kucheza mechi nje ya nchi, kuna kazi kubwa imefanyika. Kuna mambo mengi yamefanyika ili kufanikisha safari hizo.

Tena kuna timu zinaanza kupeleka watu kwa ajili ya kukodi hoteli, uwanja wa mazoezi, basi la timu na vitu vingine vinavyofanana na hivyo. Halafu baadaye timu nayo ndiyo inakwenda.

Vitu vyote hivi vinahitaji uzoefu kwenye masuala ya soka, lakini pia vinagharimu pesa nyingi.

Nadhani sasa tutaanza angalau kuanza kuwaheshimu wawekezaji. Kuna tabia imezuka kwa baadhi ya mashabiki wa soka nchini kuwabeza wawekezaji na kuwaona kama wanyonyaji wanaokuja kujipatia pesa kwenye klabu hizi za Tanzania. Utashangaa kuwa klabu za Tanzania mpaka sasa bado hazijaanza kuzalisha kitu chochote, au kujiendesha kibiashara, lakini kuna baadhi wanadai eti klabu hizi ni tajiri na zinaweza kujiendesha bila kuwa na wawekezaji. Ni kichekesho.

Kama klabu za Ulaya, ambazo zenyewe zinajiendesha kibiashara kwa asilimia 100, bado zinakubali wawekezaji tena kutoka nje ya nchi zao na hata bara lao la Ulaya, huku wakiwaheshimu, itakuwa Tanzania?

Kwanza kabisa wawekezaji wenyewe wa Tanzania ni wachache mno, kwa sababu matajiri wengi hawataki kuwekeza kwenye soka la hapa kwa sababu bado halilipi, lakini hawa hawa wachache bado wanaonekana kupigwa vita.

Klabu za Simba na Yanga zipo kwa miaka 80 sasa, lakini hazina lolote la maana zaidi ya kuwa na mashabiki wengi ambao kazi yao ni kutambiana tu mitaani kwa kuvifunga vitimu vidogo vya ndani.

Wameingia wawekezaji na kuanza angalau kusajili wachezaji wenye uwezo, kiasi cha kuanza kutamba kimataifa, wanatokea watu na kuanza kuponda. Sasa nadhani tumeanza kupata picha kuwa tukiona klabu hizi zikishiriki michuano ya kimataifa, zimesafiri iwe kwa ndege ya abiria au ya kukodi tuwaheshimu na kuwalinda wanaoziwezesha badala ya 'kuwapiga mawe'.

Kwa upande wa serikali ambayo tayari imeshakubali klabu za Tanzania kuwa na wawekezaji na ununuaji wa hisa, bado iendelee kuweka mazingira bora na mazuri kwa wawekezaji, ili aibu kama hii ya Biashara United isitokee tena.

Kwa wadau wa soka naona sasa tupunguze kelele kwa sababu hata hizi klabu za Simba na Yanga wakiondoka hawa watu tunaoona wanazinyonya, hazitotofautiana na Biashara United.

## HABARI KITAIFA

# Bil. 2.2/- kuandaa mbegu za alizeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 2.2 za kuandaa mbegu za alizeti kwa ajili ya kuinua sekta ya kilimo cha zao hili, ili kupunguza uhaba wa mafuta nchini.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, alisema walipanga kupata tani 5,000 lakini wamefanikiwa kupata tani 1,600 za mbegu hizo.

Alisema hii ni mara ya kwanza serikali imetekeleza upatikanaji wa mbegu hizo na kwamba ni muhimu kila mkulima akapata mbegu hizo kwa bei rahisi.

"Mbegu hizi zitakuwa zinapatikana katika halmashauri na kwa bei rahisi ili kuokoa fedha zinazotumika kwa ajili ya kununua mafuta," alisema Prof. Mkenda.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha mwakani hawaagizi tena mbegu nchini Ufaransa, wanahitaji kuona mbegu bora zinapatikana hapa nchini, kwa kuwa serikali hutumia zaidi ya nusu trilioni kuagiza mafuta nje.

Kwa mujibu wa Prof. Mkenda, wameteua mikoa mitatu ambayo italima alizeti chini ya usimamizi mzuri ili yaweze kuzalisha mbegu za alizeti.

Aidha, waziri huyo aligawa mbegu kwa wakuu wa wilaya na kwamba zitapelekwa kwenye halmashauri kwa ajili ya kwenda kuwauzia wananchi ambao ni wakulima. Mbali na hilo alisema wameongeza fedha za mafunzo kwa maofisa ugani na mabwana shamba, ili waweze kuwapa maelekezo mazuri wakulima.

Pia wameongeza fedha kwa ajili ya mafunzo maofisa ugani na mabwana shamba ambazo ni kutoka Sh. milioni 16 hadi bilioni 11.

Waziri huyo alisema wataendelea kuyapa kipaumbele mazao ya pamba, michikichi, karanga na mengine ili kumaliza uhaba wa mafuta nchini.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, alisema wetenga zaidi ya ekari 800,000 mkoani humo na kwamba kila wilaya itapata ekari zake kwa ajili ya kupanda mbegu hizo.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mkunda, alimhakikishia Waziri wa Kilimo kuwa mbegu hizo zitatumzwa vizuri na wakulima wote watazipata. Mkunda ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema kilio cha wakulima wa alizeti kitazidi kukua nchini.

Naye mkulima Stephen Marriale akizungumza kwa niaba ya wakulima wenzake aliishukuru serikali ka mabadiliko kwenye sekta ya kilimo inayogusa maisha ya watu wengi vijijini.



Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto), akiongozana na mwenyeji wake ambaye ni Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Abdulaziz bin Salman Al Saud, baada ya kumaliza kikao chao kilicholenga kudumisha uhusiano katika sekta ya nishati na kuwasilisha ujumbe wa Rais Samia kwa Serikali ya Saudi Arabia. **PICHA: MALIKI MUNISI**

# Mamia wajitokeza kupima macho Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imezipongeza Hospitali za CCBRT na Polisi Kilwa Road kwa kushirikiana kutoa huduma bure ya upimaji wa macho kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam katika kuadhimisha Siku ya Macho Duniani.

Akizungumza katika kuadhimisha siku hiyo, iliyofanyika kwenye eneo la Hospitali ya Polisi Kilwa Road katika Manispaa ya Temeke, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo katika hotuba yake iliyosomwa na Katibu Tarafa wa Chang'ombe, Sadath Mtware mbali ya kutambua mchango mkubwa CCBRT katika upimaji na utoaji ushauri juu ya magonjwa mbalimbali ya macho, alizitaka taasisi hizo mbili kuwa na ushirikiano endelevu kwa manufaa jamii nzima ya Watanzania.

"Kabla sijaendelea na hotuba yangu napenda kuchukua fursa hii kuzipongeza hospitali hizi mbili kushirikiana kutoa huduma hii kwa Watanzania hasa wakazi wa Wilaya ya Temeke, hili ni jambo la msingi sana na niseme mmetekeleza kwa vitendo, maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Jokate katika hotuba yake. Alizitaka taasisi nyingine katika wilaya yake ya Temeke kuangalia uwezekano wa kuunganisha nguvu na wadau mbalimbali ili kupanua wigo wa utoaji wa huduma kwa wananchi wilayani na sehemu nyingine nchini ambako uhitaji wa huduma hiyo ni mkubwa.

"Nimefurahishwa na kauli mbiu ya mwaka huu inayosema 'Yapende macho yako, Nenda kapime sasa, kila mtu anahusika' kwani inalenga kutuonyesha sisi kama jamii kutambua umuhimu wa afya na ubora wa macho," alisema na kuongeza kuwa kila mmoja na hasa watu wasiokuwa na tabia ya kupima afya ya macho yao kujenga tabia ya kupima.

Alisema CCBRT imetoa mchango mkubwa katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa afya ya macho 2018- 2022, ambao unalenga kuwa na jamii yenye afya bora ya macho ambayo pia itawezesha maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Nafahamu vizuri kuwa CCBRT mbali ya kuwa hospitali bobezi ya macho wanatibu pia magonjwa mengi tofauti na macho," alisema na kuhamasisha wanatemeke kujitokeza kwa wingi kupima afya ya macho. Awali akimkaribisha Jokate, Ofisa Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi, alisema taasisi yake na Hospitali ya Polisi Kilwa Road zina ubia wa kufanya kazi pamoja katika kutoa huduma ya macho kwa Watanzania na kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja pekee wagonjwa zaidi ya 300 wameshapata huduma ya afya ya macho.

"Kama mnavyofahamu CCBRT ni mdau mkubwa wa afya ya macho hapa nchini kwa mwaka hospitali yetu huona wagonjwa wa macho takribani 64,000, hivyo napenda kutoa wito kwa Watanzania wenzangu hasa wakazi wa Temeke na maeneo ya jirani kuchangamkia fursa ya huduma za macho zinazotolewa kwa ushirikiano baina ya hospitali zetu hizi mbili ili kwa pamoja tuweze kuzuia au kupunguza upofu unaozuilika miongoni mwetu," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**
**Usimamiz wa Mirathi Na. 16/2021**
**Raphael Joseph Bahari..............................Marehemu**
**Aba Joseph Bahari.....................Msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA**
**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi.

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 22th Novemba, 2021

Imetolewa na Hakimu Mkazi leo siku ya tarehe 22nd Octoba, 2021.






**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, CAP 117 RE 2019**
**DEEP POLL**
**BY THIS DEED, I NDEMFOO KUNDAEL FANUEL of P.O. Box 14, Songea Tanzania, formerly known as NDEMFOO KUNDAEL LYIMO DO HEREBY ABSOLUTELY renounce and abandon the use of my former name of NDEMFOO**

KUNDAEL LYIMO and in lieu thereof assume the name of NDEMFOO KUNDAEL FANUEL and in pursuance of such change of name as aforesaid, I hereby declare that I shall, at all times hereafter, in all records deeds and instruments whatsoever use and sign the said names of NDEMFOO KUNDAEL FANUEL as my name in lieu of my former name of NDEMFOO KUNDAEL LYIMO so renounced.

AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST all person to designate and address me by such assumed name of NDEMFOO KUNDAEL FANUEL only.

AND I, the said NDEMFOO KUNDAEL FANUEL make this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of the Oaths and statutory Declaration Act, Cap 34 RE 2019.

IN WITNESS WHEREOF, I have executed this Deep on the 05th day of October, 2021.



# Katika Kuadhimisha Miaka 50 ya Kurejeshwa kwa Kiti Halali cha Jamhuri ya Watu wa China katika Umoja wa Mataifa

Mhe. Chen Mingjian, Balozi wa China nchini Tanzania

MNAMO Oktoba 25, 1971, Mkutano wa 26 wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ulipitisha Azimio 2758 kwa idadi kubwa, ambayo iliamua kurejesha haki zote za Jamhuri ya Watu wa China katika Umoja wa Mataifa (UM), na kutambua kuwa wawakilishi wa Jamhuri ya Watu wa China ndio wawakilishi halali tu wa China katika UM. Kurudi kwa Jamuhuri ya Watu wa China kwenye UM, ambayo idadi ya watu inachukua robo ya jumla ya ulimwengu, imeubadilisha Umoja wa Mataifa kuwa shirika lenye mamlaka ya kiserikali la kimataifa lenye uwakilishi mpana zaidi. Pia inaashiria mwanzo wa enzi mpya katika uhusiano kati ya China na UM.

Kama mwanachama mwanzilishi wa Umoja wa Mataifa, China ni nchi ya kwanza ambayo mwakilishi wake alisaini Mkataba wa UM. Walakini, tangu kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa China, kiti halali cha China kilinyimwa kwa miaka 22, ambayo bila shaka ilikuwa aibu na kovu kwa haki na usawa wa kimataifa. Idadi kubwa ya nchi rafiki ambazo zinapenda amani na kutetea haki zilisimama na kuongea kwa ujasiri kwa China, wakitaka kurejeshwa kwa kiti halali cha China katika UM. Tanzania imekuwa na jukumu muhimu na imetoa mchango mkubwa katika shughuli hii.

Rais Julius Nyerere aliiona China kama "ndugu". Alisema hadharani kuwa haina msingi na ni upuuzi kwa nchi moja moja kuomba upigaji kura dhidi ya China katika UM. Chini ya uongozi wake, Tanzania imekuwa ikipendekeza kupitishwa kwa azimio la kurejesha kiti cha halali cha China katika UM kila mwaka katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa tangu 1969. Ilikuwa pia moja ya nchi 23 ambazo ziliwasilisha rasimu ya azimio la kurudisha haki halali za Jamhuri ya Watu wa China katika UM. Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania wakati huo kwa UM Dkt.Salim Ahmed Salim alishiriki katika mchakato mzima wa jaribio hili kutoka kwa kuzingatia na kuandaa azimio hadi kupiga kura na kupitishwa kwake. Kwa kuongezea, alifanikiwa kuzima jaribio la wawakilishi wa Marekani kuhifadhi kiti cha Taiwan katika UM. Taswira ya Dk Salim akiongoza kupiga makofi na kushangilia wakati azimio lilipopitishwa imekuwa wakati wa muhimu katika historia ya uhusiano wa China na Tanzania na China na Afrika.

Kutambua mchango bora wa Dk Salim katika kurudisha kiti cha halali cha China katika UM, kwenye hafla ya maadhimisho ya miaka 70 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa China, Rais wa China Xi Jinping alimpa Medali ya Urafiki, heshima kubwa zaidi ya China kwa marafiki wageni. Dk Salim ndiye rafiki pekee wa Kiafrika ambaye ameshinda heshima hiyo hadi leo.



Balozi Chen Mingjian.

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita baada ya kurudishwa kwa kiti chake halali katika UM, China imekuwa ikifanya ushirikiano wa pande zote. Imefuata madhumuni na kanuni za Hati ya Umoja wa Mataifa, na ilitetea mfumo wa kimataifa unaozingatia UM pamoja na utaratibu wa kimataifa unaoungwa mkono na sheria za kimataifa. China imekuwa mjenzi wa amani ulimwenguni, mchangiaji wa maendeleo ya ulimwengu, mtetezi wa agizo la kimataifa na mtoaji wa bidhaa za umma.

**-- China imelinda amani na usalama wa kimataifa.** Nchi hiyo ni ya pili kwa mchango mkubwa katika bajeti ya operesheni za kulinda amani ya UM, na mchangiaji mkubwa wa vikosi kati ya wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama. Tangu 1990, jeshi la China limeshiriki katika operesheni karibu 30 za kulinda amani na kutuma zaidi ya walinda amani 50,000. China imechukua sehemu nzuri katika utatuzi wa maswala ya kimataifa na ya kieneo. Imetetea haki kwa maneno na matendo, na ikakuza ujenzi wa ulimwengu kwa amani na usalama wa ulimwengu.

**- China imeleta msukumo kwa maendeleo ya kawaida duniani.** Nchi imechangia zaidi ya 30% ya ukuaji wa uchumi wa ulimwengu kwa miaka kadhaa mfululizo. Tangu kupitishwa kwa sera ya mageuzi na ufunguzi, China imeinua idadi ya watu vijijini milioni 770 nchini kutoka umaskini, na hivyo kuchangia zaidi ya 70% ya kupunguza umaskini ulimwenguni. China ilifikia lengo la kupunguza umaskini chini ya Ajenda ya UM ya mwaka 2030 ya Maendeleo Endelevu miaka kumi kabla ya ratiba, na hivyo kuweka mfano mzuri kwa juhudi za kimataifa katika kupunguza umaskini.



Wajumbe wa nchi nyingi wakipiga makofi wakati wa Mkutano Mkuu wa 26 wa Umoja wa Mataifa ukipitisha Azimio 2758 la kurejesha haki zote halali za Jamhuri ya Watu wa China katika Umoja wa Mataifa, New York, U.S, Oktoba 25, 1971. **PICHA: XINHUA**

**- China imetoa mipango ya mageuzi ya mfumo wa utawala wa ulimwengu.** Kukabiliwa na mabadiliko makubwa ulimwenguni yasiyoweza kuonekana katika karne moja, Rais Xi Jinping alitoa hotuba kadhaa kwenye vikao maarufu vya UM, ambapo alipendekeza ujenzi wa jamii yenye mustakabali wa pamoja kwa wanadamu na maadili ya kawaida ya wanadamu, alijibu shida za kawaida za ulimwengu, na kuonyesha mwelekeo sahihi kwa maendeleo ya ulimwengu na ya binadamu. Katika Mjadala Mkuu wa kikao cha 76 cha Mkutano Mkuu wa UM, Rais Xi Jinping aliweka mbele "Mpango wa Maendeleo ya Ulimwenguni", ambao unakusudia kuleta maendeleo ya ulimwengu katika hatua mpya inayobainishwa na maendeleo yenye usawa, uratibu na ujumuishaji.

**- China imejenga majukwaa ya ushirikiano wa maendeleo kati ya nchi zote.** Imeshiriki kikamilifu katika ushirikiano wa maendeleo ya kimataifa chini ya mfumo wa UM. Mnamo mwaka wa 2015, Rais Xi Jinping alitangaza kuanzishwa kwa Mfuko wa Amani na Maendeleo wa China-UM wenye jumla ya dola za Kimarekani bilioni 1 kwa kipindi cha miaka 10. Mwaka jana, China ilitangaza kuwa Mfuko utaongezwa kwa miaka 10 wakati mwisho wake wa awali utakapofika 2025. Hadi sasa, zaidi ya nchi na mikoa 100 zimenufaika na Mfuko huo. China imesaini hati zaidi ya 200 za Mpango wa Ukanda na Njia na nchi 141 na mashirika 32 ya kimataifa wakati Mpango wa Ukanda na Njia unafaida faida na umepokelewa vizuri kwa umma wa kimataifa. China imetekeleza miradi elfu kadhaa kamili na mipango ya misaada ya vifaa, miradi zaidi ya 10,000 ya ushirikiano wa kiteknolojia na maendeleo ya rasilimali watu, na kutoa fursa zaidi ya 400,000 za mafunzo, na kukuza maendeleo huru na endelevu ya mataifa yanayoendelea.

**- China imekusanya nguvu za kukabiliana na changamoto za ulimwengu.** Nchi hiyo imefanya ushirikiano wa kimataifa katika vita dhidi ya UVIKO-19 kwa njia ya haraka. Ilipendekeza kuongeza jukumu la UM na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO). China imekuwa ikitimiza kikamilifu ahadi ya Rais Xi Jinping ya kufanya chanjo za China kuwa faida ya umma ulimwenguni, na itajitahidi kutoa dozi bilioni 2 za chanjo za UVIKO-19 ifikapo mwisho wa mwaka huu, ikitangaza ujenzi wa ngao ya chanjo ya ulimwengu. China imechukua hatua ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Rais Xi Jinping alitangaza katika Mkutano Mkuu wa UM kwamba China itafanya kazi kwa bidii ili kuongeza uzalishaji wake wa kaboni ifikapo mwaka 2030 na kufikia kutokuwamo kwa kaboni ifikapo mwaka 2060, kwa nia ya kukuza ujenzi wa utawala wa haki, busara, ushirika wa ushindi wa pande zote mfumo wa utawala wa mabadiliko ya hali ya hewa. Katika Mkutano wa 15 wa Mkutano wa Vyama wa Mkataba wa Viumbehai uliofanyika Kunming, China, Rais Xi Jinping alitangaza mpango wa China wa kuanzisha Mfuko wa Viumbehai anuwai wa Kunming na kuongoza kwa kuwekeza Yuan bilioni 1.5 (karibu dola milioni 233 za Kimarekani) kwenye mfuko huo, ili kusaidia ulinzi wa viumbehai katika nchi zinazoendelea na kujenga nchi ya kuishi kwa umoja kati ya mwanadamu na Asili.

China haitasahau kuwa ni idadi kubwa ya nchi zinazoendelea ambazo ziliiwezesha kurejesha kiti halali katika UM. China inaahidi kufanya kazi pamoja na vikosi vyote vinavyoendelea ulimwenguni, milele kusimama na nchi zinazoendelea na kusimamia haki ya kimataifa kwa kura yake katika Umoja wa Mataifa. China iko tayari kuendelea kusaidiana na Tanzania na nchi zingine zote zinazoendelea juu ya maswala yanayohusu masilahi ya msingi ya mtu mwingine na shida kubwa, na kuimarisha mawasiliano juu ya mambo muhimu ya kimataifa na ya kikanda ili kutetea umoja wa kweli pamoja na kufuata haki zaidi na usawa wa kimataifa.




Msaada wa China wa Chanjo ya Sinovac ya COVID-19 na sindano ukiwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume huko Zanzibar, Tanzania, Julai 31, 2021. **PICHA: XINHUA**

1971-2021
中华人民共和国恢复联合国合法席位50周年
THE 50TH ANNIVERSARY OF THE RESTORATION OF THE LAWFUL SEAT OF THE PEOPLE'S REPUBLIC OF CHINA IN THE UNITED NATIONS

# Kuyaishi Maono: Kutathmini uhusiano wa kipekee wa China na Tanzania katika miaka 60

Mnamo Oktoba 25, 1971, Azimio 2758 la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa lilipigiwa kura na kupitishwa na idadi kubwa ya kura 76 zilizoidhinishwa, 35 za kukataa na 17 za kutochagua upande wowote. Azimio hili lilitambua wawakilishi wa Jamuhuri ya Watu wa China (PRC) kama "mwakilishi halali tu wa China kwenye UN".

Mtu anaweza asijue ni kwanini Tanzania iliunga mkono kwa nguvu kirejeshwa kwa kiti cha PRC katika Umoja wa Mataifa. Watu wengi waliamini hii haiwezi kutokea. Makala haya yatavijulisha vizazi vya vijana historia ya urafiki kati ya China na Afrika. Hakika imekuwa miaka sitini tangu Tanzania na China zianzishe Ushirikiano wa Maendeleo. Wakati wa uhuru wa Tanganyika, China ilianzisha uhusiano wa kidiplomasia na iliyokuwa chini ya uangalizi wa Uingereza mnamo Desemba 09, 1961. Baadaye, Zanzibar iliingia katika uhusiano wa pande mbili na China mnamo Desemba 11, 1963. Baadhi ya waangalizi wanaona kwa usahihi kuwa China na Tanzania zimekuwa katika uhusiano.


Kihistoria, uhusiano kati ya Tanzania na China umejikita katika kutetea miradi endelevu ya Maendeleo ya Uchumi na kuimarisha ushirikiano kati yao. Mapema miaka ya 1970 kwa mfano, China ilisaidia ujenzi wa Reli ya Tanzania - Zambia (TAZARA), ikiunganisha Zambia isiyokuwa na bahari na kuungana na bandari ya jiji la Dar es Salaam. Kati ya 1970 na 1975, PRC ilitumia fedha, nguvu kazi na uwezo wa kiufundi kuhakikisha kuwa reli ya km 1,860 imekamilika. Kuzungumzia nguvu kazi, China ilijitolea hadi kufikia watu 56,000 kufanya kazi kwenye mradi huo kwa kushirikiana na wafanyikazi wa Tanzania na Zambia. Kupitia mradi huu, China ilipoteza wataalam na mafundi 47 wa reli. Miaka ya hivi karibuni imeshuhudiwa kukamilika kwa Uwanja mpya wa Mpira wa Taifa wa Tanzania (ambao sasa umepewa jina la Uwanja wa Benjamin Mkapa) na Maktaba ya kisasa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mnamo mwaka 2019, mradi wa bandari ya Bagamoyo wa dola bilioni 10 chini ya Mpango wa Ukanda na Barabara ulikwama lakini tangu Juni mwaka huu umekuwa ukiijadiliwa upya ili kurekebisha masharti yake.

Kwa njia ya kipekee, China na Tanzania zimeingia Makubaliano ili kuwezesha utekelezaji wa mikataba kadhaa ya makubaliano ya ushirikiano. Kwa mfano, katikati ya mwaka 2021, Ubalozi wa China nchini Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango ya Tanzania zilitia saini Mkataba wa Ushirikiano wa kuipatia Tanzania msaada wa bure wa Wachina kusaidia miradi ya ujenzi ambayo imejadiliwa na kupitishwa na China na Tanzania. Mtindo huu wa ufadhili wa maendeleo ulimaanisha kuwa miradi ya ushirikiano itakuwa na utekelezaji mzuri na wa haraka kuliko wakati ambapo hakukuwa na mchango wa kusaidia kutoka kwenye fedha za umma.

Kwa mtiririko huo, maono ya maendeleo ya China yanajifungamanisha na ulimwengu. Katika mkutano wa viongozi wa COP-15, Rais wa China Xi Jinping alitoa wito kwa jamii ya kimataifa kuongeza ushirikiano, kujenga makubaliano na nguvu ya pamoja kulinda maisha ya dunia, akibainisha kuwa viumbe hai hufanya dunia kuwa na nguvu na uhai, na vinaweka msingi wa uhai wa binadamu na maendeleo. Kwa njia hiyo hiyo, andiko lililotolewa hivi karibuni la Beijing: ' Uhai na maendeleo ya China. Safari Ndefu ya China kutoka Umaskini hadi Ustawi' linasisitiza kwamba China inazingatia ukuaji wake nyumbani katika muktadha wa maendeleo ya kawaida ya wanadamu wote, na kuongeza kuwa maendeleo ya watu wa China lazima yawe sanjari na maslahi ya kawaida ya watu wote ulimwenguni.

Cha kufurahisha, takwimu za Benki ya Dunia zinathibitisha kuwa China imewaondoa mamilioni ya wakazi wake vijijini kutoka kwenye umasikini na kwamba idadi hiyo inachangia zaidi ya asilimia 70 ya jumla ya ulimwengu. Chakupongeza, China imefikia lengo la kumaliza umaskini lililowekwa katika Ajenda ya UN ya Maendeleo Endelevu kabla ya 2030 ilivyopangwa. Haishangazi, China kwa pamoja inasherehekea miaka 100 ya kuanzishwa kwa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), na vile vile nusu karne ya kurudishwa kwa haki zake halali katika Umoja wa Mataifa. Chakufahamu, ulimwengu unapaswa kusimama na Rais wa China ambaye anautaka 'Ulimwengu ufanye kazi pamoja kujenga jamii yenye hatima ya pamoja ya Wanadamu' kama alivyobainisha wakati alipokuwa katika Ofisi ya UN huko Geneva mnamo 2017. Kwa kweli, ubinadamu lazima uwe unaunga mkono maono ya China. Tanzania ni shahidi wa kweli kwamba China inaishi maono haya!

Kila mahali, kurudi kwa China kwenye Umoja wa Mataifa kumekuwa na maana na umuhimu wake ni kuanzia kurudisha umahiri wa UN ikizingatiwa kuwa ni mmoja wa wanachama muhimu zaidi wa Umoja wa Mataifa na ina jukumu muhimu katika umoja wa dunia. Kwa ujumla, China imetetea ushirikiano wa wengi kwa miaka mingi, ikichukua jukumu la karibu katika mashirika yote ya serikali na serikali. Taarifa zinaonyesha kuwa China imesaini mikataba zaidi ya 600 ya kimataifa. Hii sio tu inaimarisha msimamo na ushawishi wake katika UN lakini pia katika mazingira ya kimataifa kwa ujumla.



Rais Xi Jinping wa China akutana na Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres huko Beijing, China, Aprili 8, 2018. **Picha: Xinhua**

Katika kushughulikia changamoto za ulimwengu, China ilichangia pakubwa katika kusaidia Mkataba wa Paris ambao unatoa suluhisho kwa mabadiliko ya hali ya hewa na maendeleo endelevu. Wakati ya Mkutano Mkuu wa 75 wa Baraza la UN, Rais Xi Jinping alitangaza malengo ya China ya kuongeza kiwango cha uzalishaji wa CO2 kabla ya 2030 na kufikia usawa wa utoaji na ufyonzaji hewa ya kaboni kabla ya 2060. China pia imejitolea kusaidia uchumi wenye changamoto kwa kusogeza mbele malipo ya mkopo ili kupunguza pengo kati ya nchi za Kaskazini na Kusini. Vivyo hivyo, vikosi vya jeshi la China vimekuwa na jukumu muhimu katika kulinda amani pande zote katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, kuonyesha dhamira ya China kuunga mkono na kuchangia operesheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa (UNPKOs) na kuongeza zaidi mabadilishano, kuaminiana na ushirikiano wa kiutendaji kati ya nchi na majirani zake.

Katika kushughulikia changamoto za afya ya umma duniani, Jamhuri ya Watu wa China imekuwa na mchango pia. Tangu kuzuka kwa COVID-19, China imetoa dozi bilioni 1.5 za chanjo na malighafi kwa nchi zaidi ya 100 na mashirika ya kimataifa. Kwa kuongezea, nchi hiyo imezindua operesheni ya dharura ya kibinadamu na kutoa vifaa vya matibabu kwa zaidi ya nchi 150 na mashirika 14 ya kimataifa. Hasa, China imeahidi kufanya chanjo zake za COVID-19 kuwa bidhaa ya umma ulimwenguni ili kuhakikisha upatikanaji wa chanjo katika nchi zinazoendelea.

Kwa kifupi, China pia imeahidi kushirikiana na jamii ya ulimwengu ili kutatua changamoto na tofauti za kidiplomasia; kuendeleza demokrasia; kusimamia maono mapya ya usalama wa kawaida, kwa kina, ushirika na endelevu; kupambana na vitisho vya usalama visivyo vya jadi; kukuza usasa wa uwezo wa utawala wa ulimwengu na mfumo, na kwa pamoja kujenga ulimwengu wa usalama kwa wote. Zaidi ya hayo, PRC iko tayari kufanya kazi na nchi zote kuimarisha mshikamano wa ulimwengu kwa njia ya faida kwa wote, na kufanya kazi kwa utulivu kwa ajili ya mpango wa uchumi wa dunia baada ya COVID na kwa pamoja kujenga ulimwengu wenye ustawi wa pamoja.

Kama Waziri Mkuu wa zamani na Mwakilishi wa Kudumu wa UN wa Tanzania wakati huo Mhe. Salim Ahmed Salim alibainisha, msaada wa Tanzania kwa ajili ya urejeshaji wa kiti halali cha PRC katika UN haukuja kwa bahati, bali, Tanzania, kutokana na imani thabiti kwamba uanachama wa China ni ufunguo wa kuifanya UN kuwa mahiri, ilitetea urejeshaji huo. Kwa miaka mingi, China imetoa michango muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Afrika na imekuwa muhimu kwa kuendeleza ukombozi wa uchumi wa Afrika

Udumu Urafiki kati ya Afrika na China!

***Makala haya yameandikwa na Chuo cha Diplomasia jijini Dar es Salaam.***




Anita Kiki Gebe, naibu mwakilishi maalum wa pamoja wa Jumuiya ya Umoja wa Mataifa-Jumuiya ya Afrika huko Darfur, akitunuku nishani ya amani ya UN kwa askari wa Kitengo cha 2 cha Idara ya Usaidizi wa Kati cha Huduma ya Helikopta ya China huko El-Fashir, Sudan, Julai 17, 2019. **Picha: Xinhua**

# Mhagama atoa wiki moja kupitia upya sheria za vijana

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira, Kazi na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amewapa wiki moja watendaji wake kufanya mapitio ya sheria na kanuni zote zinawahusu vijana ili kuzifanya ziwe rafiki na kuwafungulia milango ya mafanikio.

Mhagama aliyasema hayo jana katika hafla ya kuadhimisha miaka mitano ya JATU PLC, jijini hapa.

Alisema serikali inatambua mchango wa vijana ndiyo maana waliokwenda kuwaibua Simiyu baada ya kuona wana maono mazuri katika kuisaidia taifa na hivi sasa wanasonga mbele katika shughuli mbalimbali.

"Taifa linawathamini sana vijana ndiyo maana wamejitokeza katika maadhimisho ya JATU na kuahidi kuzisimamia changamoto walizonazo," alisema.

Alisema mapitio hayo yatafungua milango ya vijana katika shughuli wanazozifanya.

Pia, alisema vijana ni taifa la kesho na serikali inawatambua ndiyo maana ipo mstari wa mbele kuwasaidia.

Hata hivyo, aliwaomba vijana hao kutolewa sifa kwa kuwa wengi wao hubadilika wanapopata mafanikio. "Msibweteke mlipofikia ongezeni nguvu ili kupata mafanikio zaidi kwenye shughuli mnazofanya na serikali itaendelea kuwasaidia kwa kila jambo ili vijana wasonge mbele katika kilimo mnachofanya," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mnkunda, alisema kwa miaka mitano ya JATU wamefanya vitu vizuri na kuhimiza wananchi kununua hisa za JATU. Mwanahamisi alisema Dodoma wamejipanga kuhakikisha wanashirikiana na JATU kuendeleza kilimo.

"Wanasema anza na kidogo lakini wao wanaanza na kikubwa ili kuonyesha kwamba kilimo ni jadi yao," alisema.

Alifafanua kuwa wanahitaji kuona Dodoma inakuwa mfano katika ununuaji wa hisa za JATU na kuahidi watashirikiana nao kuhakikisha wanafika mbali.

## SHIVYAWATA yapania upandaji miti Chemba

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) mkoani Dodoma limejipanga kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu itakayofanyika mwaka huu wilayani Chemba kwa kupanda miti, kuunga mkono kampeni ya kuikijanisha Dodoma.

Katika maadhimisho hayo mkuu huo, Anthony Mtaka, atakuwa mgeni rasmi siku ya kilele watu wenye ulemavu na watapata fursa ya kuonyesha bidhaa mbalimbali kwenye mabanda ya maonesho.

Akizungumza na wajumbe kwenye kikao cha kamati ya maandalizi ya maadhimisho hayo, Katibu wa Shirikisho hilo, Justust Ng'wamtalima, alisema kuwa upandaji huo wa miti utaongozwa na watu wenye ulemavu kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi mbalimbali wa serikali, wadau wa maendeleo, wananchi na watumishi wa Halmashauri ya Chemba.Ng'wamtalima alitaja shughuli zingine zitakazofanyika kwenye maadhimisho hayo ni pamoja kuendesha kongamano ambalo litakalojadili masuala mbalimbali ya watu wenye ulemavu.

"Tarehe 01.12.2021 tutapanda miti ipatayo 200, na tarehe 02.12.2021 kutafanya kongamano na siku ya tarehe 03.12.2021 siku ya kilele Mkuu wa mkoa wa Dodoma atafunga maadhimisho hayo.

"Kwa mwaka huu tunatarajia washiriki wa maadhimisho hayo ya Siku Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu watakuwa 500 wakiwamo walemavu, viongozi wa serikali, wadau wa maendeleo na jamii ya Chemba," alifafanua katibu huyo.

Aliziomba taasisi, mashirika mbalimbali wadau wa maendeleo na watu binafsi kuwa na moyo wa kuchangia maadhimisho hayo kwa kutoa fedha na mali kwa lengo la  kufanikisha kwa ufanisi zaidi




Meneja Uhusiano wa Kampuni ya simu ya Vodacom Tanzania Plc, Alex Bitekeye (kushoto), akitoa maelezo kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai,  kuhusu huduma na bidhaa mbalimbali zinazotolewa na kampuni hiyo wakati alipotembelea banda la Vodacom kwenye maonyesho ya Wiki ya Azaki, yaliyoanza  jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yahimizwa kuchunguza saratani hatari via vya uzazi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kwa kushirikiana na Asasi nne Zisizo za Kiserikali (NGO), wanaendesha kampeni maalumu waliyoipa jina; 'Afya Kwanza' ili kuhamasisha jamii kujijengea utaratibu wa kujichunguza mara kwa mara aina tatu za saratani zinazoonekana kuwa hatari kwa jamii kwa sasa za matiti, mlango wa kizazi na tezi dume.

Kampeni hiyo inaendeshwa kwa kutoa huduma ya uchunguzi wa kupima bure, kutoa ushauri na wale wanaoonyesha viashiria vya saratani hizo wanaingizwa katika programu maalumu ya kupata tiba hospitalini.

"Tunapima kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) na wale wanaoonyesha kuwa na viashiria vya saratani hizo wanapewa rufani ya kwenda kuchunguzwa zaidi ili wapatiwe huduma ya matibabu," alisema Mkurugenzi wa Kampuni ya Inspire Consultants LTD, Nseya Kipilyango, ambayo ndiyo inayosimamia mradi huo wa Afya Kwanza. Kipilyango alisema, lengo la kampeni hiyo ni kuhamasisha jamii kuweka kipaumbele cha kuchunguza afya zao, hasa saratani za via vya uzazi, ili kutibiwa mapema kama njia ya kujihakikishia kupona kirahisi.

"Mara nyingi magonjwa haya ya saratani ukiyagundua mapema yanatibika kirahisi na mtu kupona kabisa. Ila mgonjwa akichelewa kupatiwa tiba ni hatari maana tiba zake zinakuwa ni za muda mrefu na ni rahisi kupoteza maisha. Ndiyo maana tunahamasisha watu kupima hata kama hawana tatizo lolote ili kugundua mapema na kupata tiba," alisema Kipilyango.

Alisema kampeni hiyo inaendeshwa kwa wanawake wanaofika wanachunguzwa saratani ya matiti na mlango wa kizazi na kwa upande wa wanaume wanachunguzwa iwapo wana tezi dume.

"Katika miaka ya nyuma wanaume wengi walikuwa wanasita kuchunguzwa tezi dume kwa kuwa vifaa vilivyokuwa vinatumika vilihitaji kuingizwa njia ya haja kubwa," alisema Kipilyango akifafanua:

"Lakini kwa sasa tunatumia njia rahisi ya kutumia vipimo vya haraka vya damu ambavyo havitofautiana na vile vya kisasa vya kuchunguza malaria."

Mbali na kampuni ya INSPIRE, NGO zinazoshiriki kwenye kampeni hiyo ni Mashujaa wa Saratani ambao wanahudumia wagonjwa ambao tayari wameanza tiba na GENESIS ambayo inahakikisha wanaogundulika wanakuwa kwenye utaratibu mzuri wa kupata tiba.

Ametaja asasi nyingine kuwa ni Associazone Ruvuma Olnus Tanzania (ARO-T) ambao wametoa vifaa pamoja na gari maalumu lenye maabara na vipimo na kwa upande wa ORCI, ambao wanaiwakilisha serikali, wametoa wataalamu wa kupima na kutoa ushauri.

Katibu wa ARO-T, Happy Rwechungura, alisema kuwa wakazi wengi wa Jiji la Dar es Salaam wamejitokeza kwa wingi kupima katika maeneo mbalimbali waliyofika.

Alisema kampeni hiyo ilianza Oktoba 8 eneo la Mikocheni, wilayani Kinondoni na baadaye Mbagala wilayani Temeke na mwishoni mwa wiki walikuwa Kigamboni.

"Tunatazamia kuanzia kesho (leo) tutatoa huduma hiyo Kimara, Wilaya ya Ubungo na tutamalizia kampeni hiyo eneo la Kawe, wilayani Kinondoni," alisema Happy.

Nipashe
Spotika



PEA 10 YA WACHEZAJI MARAFIKI KWENYE SOKA UK. 12 - 13



# TOFAUTI 5 KATI YA MESSI NA RONALDO

**LONDON,** England

LIONEL Messi na Cristiano Ronaldo wametawala mazingira ya mpira wa miguu kwa miongo miwili kama vile hakuna wengine. Wawili hao ambao ni wapinzani wakubwa kwenye soka, walichomoza katikati ya miaka ya 2000, wana jumla ya tuzo 11 za Ballon d'Or kwa pamoja, viatu kumi vya Dhahabu Ulaya, na mataji tisa ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kati yao.

Wote wawili wana rekodi nzuri za kufunga mabao. Ni wachezaji wa mchezo mkubwa na wamekuwa wakifanya tofauti kwa klabu na nchi kwa miaka kadhaa sasa. Muhimu zaidi, wameonja mafanikio katika kiwango cha klabu na kimataifa, na kuwafanya kuwa wachezaji bora zaidi katika historia ya mpira wa miguu duniani.

Licha ya kufurahia kiwango sawa cha mafanikio kwenye mchezo huo, Messi na Ronaldo kuna vitu vingi hawafanani kabisa. Kuna mambo mengi ambayo huwatofautisha wawili hao.

Kwenye makala haya tunaangalia tofauti zao tano, zifahamu hapa...

#### #5. MBINU ZA KIMCHEZO

Jambo moja kubwa linalomtofautisha Messi na Ronaldo ni mbinu ya mchezo. Kwa miaka mingi, tumeshuhudia wawili hao wakitumia mbinu tofauti kabisa.

Ronaldo ni mshambuliaji wa moja kwa moja, wa haraka na mkali ambaye anaweza kuumiza safu ya ulinzi wa upinzani kwa urahisi zaidi kutokana na staili yake. Ronaldo anafanikiwa zaidi wakati anapotokea upande wa kushoto akikimbia kwa kasi kuelekea eneo la boksi na kutengeneza hatari.

Kwa upande wa Messi ana mtindo wa kiufundi zaidi. Nahodha huyo wa zamani wa Barcelona anategemea uwezo wake binafsi wa kumiliki mpira na kupiga chenga kuelekea eneo la hatari. Yeye pia hupenda kuingia eneo la sanduku, lakini akitokea upande wa kulia.

#### #4. UWEZO WA KUMALIZIA/STAILI YA KUSHAMBULIA

Messi na Ronaldo bado ni wachezaji wawili ambao wanaogopwa zaidi wanapokuwa eneo la hatari. Mreno huyo ana wastani mzuri zaidi wa kufunga bao kwa mchezo.

Wote wawili kila mmoja amefunga mabao zaidi ya 700 kwa kipindi chao cha uchezaji.

Wakati Ronaldo ni mwepesi zaidi wa kumalizia na kufunga bao, Messi anafunga na mara nyingine kutengeneza nafasi ya kufunga kwa mchezaji mwingine.

Ronaldo anafanya kazi kama mchungaji katika sanduku, akitumia fursa, wakati Messi mara kwa mara huangalia nani aliyepo kwenye nafasi nzuri ya kufunga na humtengeneza pasi nzuri. Ukweli ni kwamba staili ya Ronaldo ina msaada mkubwa wa kuhakikisha timu inapata mabao, tofauti na Messi.

#### #3. UWEZO WA MGUU DHAIFU

Hii ni moja ya tofauti kubwa kati ya Messi na Ronaldo. Mmoja hutegemea mguu wake wa kushoto ambao hauwezi kuzuiliwa kuvunja ulinzi wa upinzani, lakini mguu wake wa kulia hauna ubora huo.

Kwa mujibu wa takwimu, mshambuliaji huyo wa PSG anafunga mabao nane kati ya kumi kwa mguu wa kushoto, wakati anafunga bao moja tu kati ya nane kwa mguu wa kulia.

Ronaldo anafunga zaidi kwa mguu wa kulia, lakini ana uwezo mkubwa wa kufunga kwa mguu wa kushoto.

Kitakwimu raia huyo wa Ureno amefunga mabao 790 katika maisha yake ya soka, huku 145 akifunga kwa mguu wa kushoto.

#### #2. UWEZO ANGANI

Ronaldo anatawala kabisa eneo hili. Kwa kweli Messi hana uwezo mkubwa kwenye eneo hili, huku urefu wake ukiwa ni mita 1.69, ikilinganishwa na mwenzake ambaye anasimama mita 1.87.

Kwa kuongezea, Mreno huyo ana uwezo mkubwa wa kuruka juu na kufunga mabao kwa kichwa.

Kwa takwimu, Messi amefu mais nga mabao 26 ya kichwa katika ha yake ya soka, wakati Ronaldo amefunga mara 137 kwa kichwa.

#### #1. UCHEZAJI KITIMU

Linapokuja suala la kuchambua jinsi Messi na Ronaldo wanavyocheza kitimu, ni wazi kuna tofauti kubwa sana kati yao. Raia huyo wa Argentina ni wazi kwamba ni mchezaji anayecheza sana kitimu na hupenda kuunganisha timu nzima.

Messi ni mtu anayeunganisha timu kuanzia nyuma hadi mbele. Anashuka chini kupanga uchezaji wa timu yake kabla ya kusonga mbele kubadilishana pasi na washambuliaji.

Ronaldo ni mchezaji wa kibinafsi anayeweza kusaidia timu kwa uwezo wake binafsi hata kama timu yake inacheza vibaya. Tofauti na Messi, supastaa huyo wa Manchester United ana ushiriki mdogo katika kujenga uchezaji, kwani hutumia muda mwingi kuzunguka sanduku la upinzani.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa PSG, Kylian Mbappe, ndiye mchezaji wa tatu kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona, baada ya Faustino Asprilla kwa Newcastle na Andriy Shevchenko kwa Dynamo Kyiv (wote mnamo mwaka 1997).



## Extra Time

# PEA 10 YA WACHEZAJI MARAFIKI KWENYE SOKA



**LONDON,** England

MPIRA wa miguu umekuwa mchezo wa kushirikiana, uhusiano, na urafiki. Kawaida, wachezaji katika klabu moja au nchi, wana urafiki wa jumla na kila mmoja. Baada ya yote, hucheza pamoja na kufanya mazoezi pamoja karibu kila siku.

**Lakini mara kwa mara, mchezaji anaweza kuwa na urafiki wa karibu na mwenzake, kwamba, urafiki wao hauathiriwi sana hata kama watakuwa katika klabu tofauti.**

Mashabiki wa Liverpool watakumbuka ushirikiano ambao Xabi Alonso na Steven Gerrard walikuwa nao katika kipindi cha miaka mitano waliyotumia kusimamia dimba la kati la 'Wekundu' hao. Sehemu ya uzuri wao, mafanikio, na uhusiano wao ndani na nje ya uwanja huo ulitokana na kuwa marafiki wa kweli. Na urafiki wao haukufa hata wakati Alonso alipoondoka na kwenda kucheza kule Real Madrid.

Kwa Zlatan Ibrahimovic na nyota wa zamani wa kimataifa wa Brazil, Maxwell, kutengana hakukuja kuwa rahisi baada ya kuanza kucheza pamoja kule Ajax. Urafiki wao uliongezeka na wakaishia kucheza pamoja Inter Milan, Barcelona, na Paris Saint-Germain.

Ibrahimovic bado anaendelea kucheza nchini Italia, wakati Maxwell ni mkurugenzi wa michezo pale PSG, lakini wawili hao hawajapoteza mawasiliano.

Kuna hadithi zingine nyingi za urafiki wa kushangaza kati ya wanasoka ambao huchukuwa miongo kadhaa katika historia ya mchezo huo.

Lakini hapa tunaangalia pea 10 ya marafiki bora ambao bado wanaendelea kucheza na jinsi urafiki wao ulivyochipuka zaidi, twende sasa...

### #10. MASON MOUNT NA DECLAN RICE | MARAFIKI BORA TANGU AKADEMI YA CHELSEA

Hauwezi kuwatenganisha tangu siku zao za utoto pale Chelsea, Mason Mount na Declan Rice wameendelea kuwa marafiki wazuri ingawa leo hii wanacheza katika klabu mbili tofauti za Ligi Kuu England.

Wakati Mount akiwa pale Stamford Bridge, akiisaidia 'Blues' kupata Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Rice alijiunga na West Ham ambapo ameipeleka timu hiyo kwenye nafasi sita za juu na kufuzu kucheza Ligi ya Europa. Wachezaji wote wapo kwenye timu ya Taifa ya England ambapo wanafanya mazoezi, kucheza, na kusherehekea mafanikio yao pamoja.

Ushindi wa hivi karibuni wa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wa Chelsea ulikuwa furaha kubwa kwa Mount, na mara moja alimpigia simu rafiki yake wakati akiwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo baada ya mchezo kumalizika.

### #9. MATTHIJS DE LIGT NA FRENKIE DE JONG | MARAFIKI BORA TANGU AJAX

Wamekuwa wakifanya manunuzi ('shopping') pamoja, wakiendesha kwa pamoja kuelekea mazoezini na muda wote wanatoka pamoja. Hii ilikuwa wakati wa siku zao kule Ajax, wakati Matthijs de Ligt alikuwa bado anafikiria ofa ya Juventus na Frenkie de Jong alishafanya uamuzi wa kuhamia Barcelona.

Walikuwa hawawezi kutenganishwa wakati wakiwa katika klabu hiyo ya nchini Uholanzi, lakini hiyo haijabadilika katika miaka ya hivi karibuni. Wawili hao hucheza timu ya wakubwa ya Uholanzi na ushirikiano wao uwanjani bado ni furaha kuu.

Lakini ripoti zimeibuka juu ya nyota huyo wa Juventus kuhusu kutaka kujiunga na rafiki yake kule Barcelona. Huku miamba ya Turin ikiwa katika wakati mgumu kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, baada ya kumpoteza Cristiano Ronaldo, inasemekana mlinzi huyo wa kati anafikiria chaguo zake. Na imeripotiwa kwamba, anataka kujiunga na rafiki yake kule Catalunya.

### #8. JESSE LINGARD NA MARCUS RASHFORD | MARAFIKI BORA MANCHESTER UNITED

Wanaweza kuwa na tofauti ya miaka mitano kwa umri, lakini Marcus Rashford na Jesse Lingard walipitia hadithi inayofanana. Wote wawili walijiunga na akademi ya United wakiwa na umri wa miaka 7, na wote waliibuka na kuwa chaguo la kwanza pale Old Trafford. Leo hii wako pamoja wakati wote na hata likizo wanakuwa pamoja.

Nyota wote wawili wanacheza pia timu ya wakubwa ya England.

### #7. HARRY KANE NA SON HEUNG-MIN | MARAFIKI BORA TOTTENHAM

Wakati Jose Mourinho aliposema urafiki wa wawili hao ni muhimu kwa mtindo wao wa kucheza uwanjani, hakuwa anatania.

Wachezaji wote wameibeba Spurs kwenye safu ya ushambuliaji kwa misimu michache, lakini wakati Son ameongeza mkataba wake klabuni hapo, Kane anatafuta njia ya kutoka. Ingawa sakata lake la uhamisho linaathiri matokeo uwanjani, ni suala la muda tu kabla Kane hajaanza kuifungia tena Tottenham.

Wakati Son akiwa kwenye kiwango chake, mashabiki wa Spurs watatarajia nguvu mpya kutoka kwa wawili hao.

### #6. JOHN STONES NA HARRY MAGUIRE | MARAFIKI BORA TANGU LIGI ZA CHINI

Walianza safari yao katika timu za vijana za Sheffield United na Barnsley, na wote wamekuwa kuzichezea klabu mbili kubwa za Jiji la Manchester. Wote walikuliwa kule Yorkshire, wakiwa ni majirani.

### #5. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG NA ALEXANDER LACAZETTE | MARAFIKI BORA ARSENAL

Wawili hao walikutana Januari 2018 na tangu hapo wamekuwa maswahiba wakubwa.

Ingawa wakosoaji na wataalamu walidhani kwamba Aubameyang angeweza kuchukuwa nafasi ya Lacazette mbele, au kinyume chake, urafiki wao uliongezeka na walikuja haraka kutuliza wasiwasi wowote wa kufunga mabao.

Wawili hao waliunda ushirikiano mzuri uwanjani, wakifunga mabao 50 kati yao. Si tu washirika mahiri uwanjani, pia ni marafiki nje ya mpira wa miguu.

### #4. LUKA MODRIC NA GARETH BALE | MARAFIKI BORA TANGU TOTTENHAM

Gareth Bale na Luka Modric walitengeneza mawimbi makubwa huko Tottenham Hotspur kwa zaidi ya muongo mmoja uliopita. Walicheza mpira mzuri, lakini walikuwa marafiki wa haraka pia.

Wakati Modric alipohamia Real Madrid, hakupoteza mawasiliano na Bale, na kufikia mwaka 2013, kiungo huyo alijadili waziwazi uhamisho wa raia huyo wa Wales kutua pale Santiago Bernabeu.

Los Blancos hao walisikiliza maneno ya Modric na kumleta Bale, na miaka iliyofuata ilishuhudia wawili hao wakishinda mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ingawa Bale amekuwa katika wakati mgumu kwa siku za hivi karibuni huko Madrid, lakini bado ufariki wao umezidi kuimarika.

### #3. MARCO REUS NA ROBERT LEWANDOWSKI | MARAFIKI BORA TANGU BORUSSIA DORTMUND

Kwa Marco Reus, ilikuwa misimu michache migumu, marafiki wake wa karibu Mario Gotze na Robert Lewandowski waliondoka Borussia Dortmund kwenda Bayern Munich katika misimu miwili mfululizo.

Lakini wakati Gotze sasa anacheza PSV, Reus na Lewandowski wanaendelea na urafiki wao, wakicheza katika timu kubwa pinzani katika soka la Ujerumani.

Ingawa wanajiachia wote nje ya uwanja, huwa wanajaribu kadiri iwezekanavyo kuonekana kama maadui wakati wa mchezo. Kwa sababu wanacheza katika klabu mbili pinzani zaidi.

### #2. CRISTIANO RONALDO NA MARCELO | MARAFIKI BORA REAL MADRID

Wakati wachezaji hao wawili walipokutana, ilikuwa kwenye mchezo wa kimataifa kati ya Brazil na Ureno mwaka 2008, na waligombana. Lakini tangu Ronaldo alipojiunga na Marcelo kule Real Madrid, wawili hao imekuwa vigumu kuwatenganisha ndani na nje ya uwanja. Alipokuwa Juventus, Ronaldo alibainisha wazi kwamba, anahitaji Marcelo ajiunge naye. Familia zao pia zimekuwa marafiki wakubwa.

### #1. LIONEL MESSI NA LUIS SUAREZ | MARAFIKI BORA BARCELONA

Luis Suarez na Lionel Messi wamekuwa na urafiki maarufu, kuanzia uwanjani hadi nje ya uwanja. Lakini Suarez alionekana hahitajiki Barcelona na akahamia Atletico Madrid ambapo alitwaa taji la Ligi Kuu ya Hispania kwa kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone.

Kwa upande mwingine, Messi amejiunga na Paris Saint-Germain baada ya mkataba wake na Barcelona kumalizika. Lakini nyota hao wawili wamebakia kuwa karibu sana.

Wake na familia zao zinapata chakula cha jioni pamoja mara kwa mara kila wanapopata nafasi, ni sawa kusema kwamba wawili hao wana urafiki bora zaidi kwenye mpira wa miguu duniani.

## Nukuu

"Siwasalimii kila wakati (makocha wengine) baada ya mechi kwa sababu sipendi hilo," **Kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone, akiwaambia waandishi wa habari alipoulizwa kuhusu tukio la kukukataa kumsalimia Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, baada ya kushushiwa kichapo cha mabao 3-2 wiki iliyopita.**



"Najua wakati timu inahitaji msaada wangu kwa kujilinda. Lakini jukumu langu katika klabu ni kushinda, kuisaidia timu kushinda na kufunga mabao - [upande wa kujilinda] ni sehemu ya kazi yangu. Watu ambao hawataki kuona hiyo ni kwa sababu hawanipendi. Ninaenda kitandani kwangu na dhamiri yangu nzuri sana. Endelea na hiyo kwa sababu bado nitafunga midomo na kushinda vitu," **Mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo**



"Kwangu mimi, bado ni sawa. Bado ni mchezo bora katika mpira wa miguu. Haijalishi ni wachezaji gani wapo, nani ameondoka, au ni nani atakayejiunga. Real-Barça ni ya kihistoria. Majina hubadilika, lakini kabla kulikuwa na Zidane, Ronaldinho, Ronaldo, Eto'o. Real-Barça daima watakuwa Real-Barça," **Mshambuliaji wa Real Madrid, Karim Benzema akizungumzia El Clasico kabla ya kupigwa jana.**






Kipa Aboutwalib Mshelly wa Mtibwa Sugar, mmoja kati ya makipa wanne waliookoa penalti kwenye mechi za Ligi Kuu hadi kufikia juzi. **PICHA: MAKTABA**

# MAKIPA MASHUJAA WA PENALTI LIGI KUU 2020/22

**Na Adam Fungamwango**

KABLA ya mechi za Jumapili za Ligi Kuu, jumla ya penalti tano zilikuwa zimepatikana, huku moja tu ikiwekwa wavuni.

Shiza Kichuya wa Namungo FC, ndiye mchezaji pekee aliyefunga penalti mpaka sasa kwenye Ligi Kuu hadi kufikia Jumamosi.

Alifanya hivyo kwenye Uwanja wa Ilulu, alipoweka wavuni mkwaju wa penalti, akiisawazishia Namungo FC, iliyokuwa inaongozwa kwa bao moja dhidi ya KMC.

Bao hilo liifanya timu hizo kufungana 1-1, hivyo penalti nne zilizobaki zilikoswa na wachezaji John Bocco wa Simba, Eliud Ambukile wa Mbeya City, Boban Zirintusa wa Mtibwa Sugar na Raymond Masota wa Geita Gold.

Penalti zote hizi ziliokolewa kwa ustadi na makipa, hapa tunakuletea magolikipa waliookoa penalti hizo, jinsi walivyookoa na mechi walizocheza, haya sasa...

**#1. JAMES SSETUBA - BIASHARA UNITED**

Kipa huyo raia wa Uganda, aligeuka shujaa alipookoa penalti ya nahodha wa Simba, John Bocco kwa kuruka upande wa kulia na kupangua. Ilikuwa ni dakika ya tatu ya nyongeza kwenye moja ya mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu kati ya Biashara United na Simba, ukichezwa Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Baada ya Pape Sakho kuangushwa ndani ya eneo la hatari, ilionekana kama Simba ingeweza kupata bao kwenye mechi hiyo iliyochezwa Septemba 28, mwaka huu, lakini kipa huyo alifuta matumaini hayo, timu hizo zikatoka sare ya bila kufungana.

**#2. HAMAD JUMA - MBEYA KWANZA**

Kipa wa Mbeya Kwanza, Hamad Juma alicheza penalti ya Ambukile dakika ya tatu ya mchezo wa Ligi Kuu, timu hiyo ikicheza dhidi ya ndugu zao Mbeya City, Oktoba 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya. Ni mechi ambayo iliisha kwa sare ya mabao 2-2. Kama Mbeya City ingefunga mkwaju huo ingeweza kuibuka na ushindi.

Kipa huyo aliruka upande wa kulia alikopiga mpigaji na kupangua mchomo huo, akiwaweka salama Mbeya Kwanza, pia kuwabakisha mchezoni.

**#3. KHOMEIN ABOUBAKAR - GEITA GOLD**

Kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu, Geita, kipa Khomein Aboubakar wa Geita Gold aliokoa penalti iliyopigwa na Boban Ziruntusa wa Mtibwa Sugar, Oktoba 16 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ilikuwa ni dakika ya 28, Mtibwa Sugar ilipopata penalti, lakini mpigaji ambaye alipiga upande wa kushoto, alishuhudia kipa huyo naye akiruka huko huko na kuupangua. Ni mechi ambayo iliisha kwa sare ya bao 1-1.

**#4. ABOUTWALIB MSHELLY - MTIBWA SUGAR**

Ni mechi ile ile ya Geita Gold dhidi ya Mtibwa Sugar. Ni mechi ambayo imeingia kwenye rekodi ya kupatikana kwa penalti mbili kwenye mchezo mmoja msimu huu, kila timu ikipata penalti moja. Lakini zote zilishindwa kuzitumia.

Ilikuwa ni dakika moja kabla ya mechi kumalizika, wenyeji Geita Gold walipopata mkwaju wa penalti. Wakati huo mechi ilikuwa sare ya bao 1-1. Kazi ilikuwa ni kuukwamisha wavuni, ili iondoke na ushindi wa bao 1-0.

Shughuli hiyo aliachiwa Raymond Masota. Mshelly alimuotea mpigaji na kuruka upande wa kulia, akiucheza kwa ustadi wa hali ya juu, akiwanyima wenyeji bao dakika za mwisho, akiwafanya mashabiki wa Geita Gold waliojazana kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Nyamkumbu, wakiwamo wanafunzi wa shule hiyo waliokuwa wamevalia sare, kuondoka vichwa chini.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo, hadi sasa amefunga mabao 795 yaliyotokana na mechi 1085 kwenye maisha yake ya soka, kati ya hayo, 145 amefunga kwa mguu wa kushoto huku 137 akifunga kwa kichwa, mpinzani wake Lionel Messi yeye kwa kichwa amefunga 26 tu hadi sasa.



# Bei elekezi mbegu ya alizeti yaanikwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema kilo moja ya mbegu bora ya alizeti itauzwa kwa Sh.3,500 kwa wakulima ili kuinua kilimo hicho na kukabiliana na tatizo la upungufu wa mafuta ya kula nchini.

Waziri wa Kilimo, Pro.Adolf Mkenda, aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa mpango wa usambazaji wa mbegu za alizeti kwa wakulima ambapo Sh. bilioni 2.2 zimepangwa kutumika kununua na kugawa mbegu hiyo kwa wakulima.

Alisema lengo ni kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 500 ambazo hutumika kwa mwaka kuagiza mafuta hayo nje ya nchi.

Alibainisha kuwa serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha tatizo la uhaba wa mbegu linatatuliwa miaka michache ijayo.

"Mahitaji ya mbegu za alizeti ni makubwa nchini kwa sasa zimepatikana tani 1,600 hadi 2,000 wakati mahitaji halisi ni tani 5,000," alisema.

Aliongeza: "Mbegu hizi zitakuwa zinapatikana katika halmashauri na kwa bei rahisi ili kuokoa fedha zinazotumika kwa ajili ya kununua mafuta."

Alifafanua kuwa wameteua mikoa mitatu ambayo italima alizeti chini ya usimamizi mzuri ili kuzalisha mbegu hizo kwa wingi. Kadhalika, alisema wameongeza fedha za mafunzo kwa maofisa ugani na mabwana shamba ili kuwapa maelekezo mazuri wakulima.

Pia alisema wataendelea kuyapa kipaumbele mazao ya pamba, michikichi, karanga na mengine ili kumaliza uhaba wa mafuta nchini.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa, Dk. Fatma Mganga, alisema ekari 800,000 zimetengwa kwa Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kupanda mbegu hizo.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mkunda, alimhakikishia Waziri wa Kilimo kuwa mbegu hizo zitatunzwa vizuri na wakulima wote watazipata.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Dk. Sophia Kashenge, alisema kama taasisi inaendelea kufuata maelekezo ya Wizara ya Kilimo na kuhakikisha tatizo la mbegu linakwisha.



Waziri wa Ulinzi, Dk. Stergomena Tax, akikagua gwaride lililoandaliwa maalumu kwa ajili ya maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Mataifa (UN), yaliyofanyika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma, mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Baraza lafafanua usajili madaktari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Madaktari Tanganyika limesema halitasajili mtu ambaye hajakidhi vigezo kwa mujibu wa sheria ya udaktari, udaktari wa meno na afya shirikishi sura namba 152(4).

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Prof. David Ngassapa, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari kuhusu utaratibu wa kupokea watarajali na kufanya mitihani ya baraza hilo.

Alisema baraza hilo ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na limekuwa na utaratibu wa kupokea watarajali na kuwapa usajili wa awali kwa ajili ya kuwapangia katika vituo vya utarajali kama sheria inavyoelekeza na baadaye usajili kamili wakishamaliza na kufaulu mtihani baada ya utarajali.

"Chini ya kifungu cha 20 kifungu kidogo (1) kabla ya kupata usajili muombaji anatakiwa kutimiza vigezo vilivyoainishwa, mtu hatastahili kusajiliwa chini ya sheria hiyo isipokuwa awe ameridhisha Baraza la Madaktari Tanganyika," alisema.

Alieleza kuwa anayesajiliwa anatakiwa kuwa ni mtaalamu wa udaktari, udaktari wa meno au afya shirikishi ama ana shahada ya udaktari au udaktari wa meno kutoka katika taasisi inayotambuliwa na amefaulu mtihani uliotungwa na baraza.

"Baraza limekuwa likipata maombi ya wanafunzi mbalimbali kuingia katika mafunzo ya utarajali ambao hawana uthibitisho wa kuhitimu mafunzo yao ya shahada kutoka nje ya nchi," alisema.

Kadhalika, alisema maombi hayo yamekuwa yakikataliwa na baraza kwa kuwa yanakinzana na matakwa ya kifungu 20 (1) (a) cha sheria tajwa.

"Baraza baada ya kufanya uchunguzi limegundua kuwa wanafunzi hawa wanagawanyika katika makundi matatu kundi la kwanza ni wanafunzi wa mwaka wa mwisho ambao wanakuja kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa vitendo ya mwaka wa mwisho wa masomo," alisema.

Kundi la pili alisema ni wanafunzi ambao wamemaliza masomo yao na wanavithibitisho vya kumaliza ambavyo vimethibitishwa na vyuo vikuu vinavyotambulika na tume ya vyuo vikuu.

Kundi la tatu alisema ni wanafunzi wanaosoma nje ya nchi na wakakumbana na tatizo la kushindwa kurudi vyuoni kwa sababu ya ugonjwa wa UVIKO-19.

"Kundi hili linaelekezwa kukamilisha taratibu za kumalizia masomo yao na kufanya mtihani wa mwisho ndipo warudi kujiunga na utarajali," alisisitiza Prof. Ngassapa.

# Taasisi yakuna Bunge kwa elimu wachimbaji wanawake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji Mitaji ya Umma (PIC), imepongeza Taasisi ya HakiRasirimali kwa kutoa mafunzo kwa wanawake wachimbaji wadogo wa madini zaidi ya 2,000 na kuwajengea uwezo kushiriki kwenye sekta ya madini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Atupele Mwakibete, alitoa kauli hiyo jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI).

Alisema kamati hiyo inaipongeza taasisi hiyo kwa kuwezesha wanawake wachimbaji wadogo wa madini kupata mafunzo mbalimbali ili kushiriki kikamilifu katika sekta hiyo. "Niwapongeze sana HakiRasilimali kwa jitihada mnazaozifanya za kuisaidia serikali katika kufikisha elimu kwa wananchi hadi ngazi ya chini kabisa kwani wanawake hawa pamoja na kuwapatia elimu lakini mnawatafutia masoko huko duniani."

"CSO niwapongeze sana kwanza wanakwenda moja kwa moja ambapo serikali haifiki wanasapoti hata wale ambao serikali haina bajeti nao wakati mwingine serikali inaishia mkoani au wilayani tuu, lakini CSO zinakwenda hadi ngazi ya kaya kusaidia walemavu kutoa elimu ya kutoka pale walipo," alisema.

Alitoa wito kwa serikali katika maeneo ambayo madini yanachimbwa iweke mfuko maalum kuwezesha CSO, ili kufikia wananchi katika maeneo mengi na kutoa elimu. "Maeneo mengi wenyeji hawachimbi madini kutokana na kukosa elimu ya uchimbaji, hivyo wanaonufaika nayo ni watu kutoka mbali na wao wanapata kidogo sana na hata wengine wanauza maeneo yao kupisha watu wengine kuja kuchimba," alisema.

Alisema kutokana hali hiyo serikali ingeweka bajeti kwa ajili ya mashirika ya kiraia kutoa elimu ili wananchi kutambua thamani ya madini yalipo katika maeneo yao.

"Naiomba serikali, Wizara ya Madini pamoja na kamati yangu katika bajeti ya 2022, kuweka fedha kwa ajili ya kuwezesha asasi za kiraia kutoa mafunzo kwa wananchi kwenye madini ili mtu atambue thamani ya madini badala ya kuendelea kuona madini kama chupa," alisisitiza.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa HakiRasilimali, Rachel Chagonja, alisema moja ya tatizo linalowakabili wanawake katika sekta ya uchimbaji wa madini ni mila potofu.

"Watu bado wanaamini kuwa wanamke hawezi kuingia mgodini kushiriki uchimbaji kama ilivyo kwa wanaume hii yote ni kutokana na imani potofu zilizojengeka katika jamii zetu," alisema.

Kadhalika, aliwataka wanawake kujitokeza kushiriki katika sekta za uchimbaji madini na kuacha kulalamika kuwa watengwa.

Hata hivyo, alisema rasilimali za nchi zinaweza kuwa chachu katika mpango wa maendeleo wa taifa kama wananchi pamoja na wadau mbalimbali watashirikishwa katika utungaji na uboreshaji wa sera na sheria za masuala ya madini.

HABARI KITAIFA

# Sayansi yakwamisha ajira kwa wasichana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 12 pekee ya wanafunzi wote wa kike wanaojiunga na elimu ya sekondari nchini ndiyo wanaofanikiwa kupata ajira hasa kwenye taasisi zinazojihusisha na mambo ya teknolojia kutokana na wengi wao kutopenda masomo ya sayansi.

Kwa mujibu wa takwimu zilitolewa na timu ya wafanyakazi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam (DIT), ambayo ipo jijini Mbeya kuhamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na masomo ya sayansi, idadi hiyo imepungua kutoka asilimia 52 ya wasichana wanaojiunga na elimu ya sekondari nchini.

Akitoa hamasa ya kusoma masomo ya sayansi kwa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Kutwa Mbeya, Mkufunzi wa DIT, Dk. Asinta Manyele, alisema kupungua kwa wasichana katika ajira kunakwamisha mpango wa taifa wa kufikia asilimia 50 kwa 50 kwenye vyombo vya maamuzi.

"Idadi ya watoto wa kike inapungua sana, kwa mfano wanaojiunga na elimu ya sekondari huwa ni asilimia 52 ya wanafunzi wote, lakini inapofikia hatua ya kwenda chuo kikuu wanapungua hadi asilimia 37 na kufika kwenye ajira wanabakia asilimia 12, jambo ambalo linakwamisha mpango wa kufikia usawa wa 50 kwa 50 na wanaume," alisema Dk. Asinta.

Aliwataka wanafunzi hao kueleza sababu zinazowakwamisha kusoma masomo ya sayansi na kusema serikali ipo tayari kushughulikia changamoto zote walizonazo ili waweze kujiunga na masomo ya sayansi.

Baadhi ya walimu wanaofundisha masomo hayo, walisema kuna mambo mengi yanayochangia wanafunzi wa kike kutopenda kusoma masomo ya sayansi.

Mwalimu Agusta Kinemo, anayefundisha somo la Fizikia katika Shule ya Sekondari Sinde jijini hapa, alisema uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi ni sababu kuu inayowaondoa wanafunzi wengi hasa wa kike kupenda kusoma sayansi.

Alisema kutokana na uhaba wa walimu, wanafunzi hawafundishwi vyema masomo hayo na hata wanaobahatika kufundishwa, hawapati elimu hiyo kwa wakati jambo ambalo linasababisha wayaone masomo ya sayansi magumu na kutoyapenda.

Mwalimu Kinemo alisema sababu nyingine ni uhaba au ukosefu wa zana bora za kufundishia, jambo ambalo linawafanya wanafunzi washindwe kuyaelewa vyema masomo hayo.

Baadhi ya wanafunzi walisema elimu waliyoipata kwenye kikao hicho imewapatia hamasa kubwa ya kupenda masomo ya sayansi na kuanzia sasa wataanza kuyasoma kwa bidii.

Devotha Emmanuel ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya Mbeya Day, alisema kabla ya kupata elimu hiyo alijua wenye uwezo wa kusoma masomo ya sayansi ni wavulana, lakini sasa ametambua kuwa hata wasichana akiwamo yeye mwenyewe wanaweza kusoma na kufaulu vizuri masomo hayo.



Mwakilishi wa Mradi wa SAWA unaotekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF), Joachim Asenga, akimkabidhi vifaa vya kufanyia usafi kwenye shule za msingi, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Maji wa Tunduma, Franco Ngonya, mwishoni mwa wiki wakati wa uhamasishaji wa usafi katika Shule ya Msingi Makambini. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waagizwa kuanzisha klabu utunzaji mazingira

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

HALMASHAURI ya Mji wa Tunduma katika Wilaya ya Momba, mkoani Songwe, imewaagiza maofisa elimu wa kata zote 15 za mji huo kuanzisha klabu za utunzaji wa mazingira kwenye shule zote za msingi kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi kutunza mazingira.

Klabu hizo zimetakiwa kuundwa ili kuyaweka mazingira kuwa safi na kuepuka magonjwa ya mlipuko ikiwamo kuelimishana ikiwamo ugonjwa wa Uviko-19 ambao unautesa ulimwengu kwa sasa.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Franco Ngonya, wakati wa utoaji wa elimu ya unawaji kwa wanafunzi katika Shule ya Msingi Makambili, mjini humo zoezi ambalo lilihudhuriwa pia na wadau mbalimbali.

Ngonya ambaye ni Ofisa Elimu, Vifaa na Takwimu wa Halmashauri ya Tunduma, alisema utekelezaji wa agizo hilo itakuwa ni moja kati ya vipimo vya utendaji kazi wa maofisa elimu wa kata za mji huo.

Alisema kila ofisa anatakiwa kusimamia uundwaji wa klabu hizo na shule zote za kata zao ili ziwe na ufanisi lengo ziwe hai na zifanye kazi ya kuhamasisha usafi wa mazingira.

"Tunashukuru kumekuwa na mwitikio mzuri wa wadau kuja kutoa elimu hii, sasa niwahakikishie kwamba zoezi hili litakwenda vizuri sana, maagizo haya niliyotoa kwa maofisa hawa litakuwa kipimo kwao," alisema Ngonya.

Wadau wa mazingira likiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wake wa SAWA, waliomba serikali kuendelea kuwajengea watoto tabia ya usafi ikiwamo kunawa mikono kila wakati wakiwa bado wadogo.

Mwakilishi wa Mradi wa SAWA, Joachim Asenga, aliiomba serikali kuhakikisha maji yanapatikana katika kila shule ili wanafunzi wanapofundishwa wafundishwe pia kwa vitendo badala ya kufundishwa kwa nadharia.

Alisema ni miongoni mwa shule ambazo shirika hilo liliziwezesha kujenga vyoo vya kisasa na kutoa elimu ya usafi wa mazingira kwa wanafunzi hali iliyosaidia kuboresha mazingira ya shule hiyo.

Alisema ili kuendeleza hali hiyo ya usafi, Halmashauri ya Mji wa Tunduma inatakiwa kuongeza wigo wa utoaji wa elimu ikishirikiana na wadau wengine pamoja na kuhakikisha kila shule inakuwa na maji ya kutosha.

"Hii shule tulibaini kuwa ilikuwa na tatizo kubwa la vyoo ndiyo maana tukaamua kujenga vyoo vya kisasa, kuweka miundombinu ya maji na kuwawekea wanafunzi maeneo ya kunawa mikono, sasa tunatamani hii elimu na miundombinu isambae shule zote," alisema Joachim.

Nao baadhi ya maofisa watendaji wa kata walisema shule nyingi katika halmashauri hiyo ya Tunduma zilikuwa na klabu za mazingira za wanafunzi, lakini zilikufa kutokana na kutotiliwa mkazo.

Mmoja wa maofisa hao, Mwalimu Martha Zacharia, alisema baada ya agizo hilo la serikali wanaenda kuzifufua ili zianze kufanya kazi kwa kuwa zilikuwa na msaada mkubwa kwenye maeneo hayo ya shule pamoja na majumbani.

Alisema wanafunzi hao walikuwa wanasaidia kueneza elimu ya usafi kwa kuipeleka nyumbani ambako walikuwa wanasisitizwa kuendelea nayo.

## Waomba kuboreshewa skimu ya umwagiliaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa Bonde la Utengule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwaboreshea Skimu ya Umwagiliaji ya bonde hilo kwa kusakafia mfereji ili kuepusha upotevu wa maji unaosababisha migogoro baina yao.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wakulima hao walisema chanzo cha skimu hiyo ambacho ni Mto Nzovwe kina maji mengi, lakini kutokana na mfereji huo kutosakafiwa mengi yanapotea njiani na kusababisha upungufu kwenye mashamba.

Mmoja wa wakulima hao, Yohana Mwazyunga, alisema wakulima wamekuwa wakigombania maji mara kwa mara kutokana na kiasi kinachofika mashambani kutokidhi mahitaji na njia pekee ya kuondoa migogoro hiyo ni kuiboresha skimu.

Alisema wakati mwingine huwa wanalazimika kuweka mgawo wa maji ili wakulima wamwagilie kwa awamu, lakini bado hayatoshelezi huku mwamko wa wakulima kulima kilimo cha umwagiliaji ukiongezeka.

"Huu mfereji una urefu wa zaidi ya kilomita 10, lakini ukisakafiwa angalau kilomita tano tatizo litakuwa limepungua kwa kiasi kikubwa, ukienda kwenye chanzo unakuta maji tuliyochukua ni mengi, lakini yanayofika huku mashambani ni kidogo sana," alisema Mwazyunga.

Naye Godlove Huruma, Mwenyekiti wa kikundi cha vijana wanaolima vitunguu katika bonde hilo, alisema wakati mwingine wanalazimika kulala mashambani ili wamwagilie usiku kwa kuwa watumiaji wa maji wanakuwa wachache.

Hata hivyo, alisema kwa sasa watu wengi wamegundua mbinu hiyo hali ambayo bado inasababisha migogoro ya kugombea maji huku akidai kuwa muda wa usiku hata usalama huwa ni mdogo.

"Humu mashambani ni hatari sana nyakati za usiku maana kama unavyojua huo ni muda ambao unaweza ukang'atwa na nyoka au hata kama una adu yako anaweza akautumia muda huo kukuvizia na kukudhuru," alisema Godlove.

Alisema baadhi ya wakulima wenye mitaji mikubwa wamekuwa wakitumia mashine kuvuta maji kutoka Mto Nzovwe, lakini kwa vikundi vya vijana kama cha kwao ambavyo havina mitaji inakuwa vigumu.





# 54,324 kufanya mtihani darasa la nne kuanzia leo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTIHANI wa Taifa wa darasa la nne Zanzibar unatarajiwa kuanza leo, ambao utawashirikisha watahiniwa 54,324 wa kati yao wanawake ni 26,745 na wanaume ni 27,579.

Mkurugenzi Baraza la Mitihani Zanzibar, Zuberi Juma Khamis, alisema idadi hiyo ni ongezeko la watahiniwa 3,372 sawa na asilimia 7.0 ikilinganishwa walioandikishwa mwaka 2020. “Mitihani ya darasa la nne itaanza Oktoba 25 (leo) hadi Oktoba 26 (kesho).

Alisema mitihani ya darasa la sita itaanza Jumatano hadi Novemba 2 na mitihani ya kidato cha pili itaanza Novemba 3 hadi Novemba 12.

Mkurugenzi huyo alisema kwa mtihani wa darasa la sita watahiniwa 47,471 wameandikishwa wakiwamo wanawake 24,755 na wanaume 22,715 na kwamba 13,253 wameongezeka sawa na asilimia 38.7 ikilinganishwa na mwaka 2020.

Aidha, alisema watahiniwa 32,957 wameandikishwa kufanya mtihani wa kidato cha pili kati yao wanawake ni 17,405 na wanaume ni 15,552 na kuwa kuna upungufu wa watahiniwa 9,165 sawa na asilimia 27.1 ikilinganishwa na idadi ya watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani huo mwaka 2020.

Alisema kati ya watahiniwa walioandikishwa, watahiniwa wenye mahitaji maalumu ni 40 kwa darasa la nne 33, darasa la sita ni 33 na wa kidato cha pili ambao mitihani yao huandaliwa kwa mujibu wa hali za mahitaji yao ili kuwawezesha kupata haki yao ya elimu.

Alieleza kuwa jumla ya wasimamizi 1,981 kwa mtihani wa darasa la nne, 1,796 kwa mtihani wa darasa la sita na 1,284 kwa mtihani wa kidato cha pili wameteuliwa kusimamia mitihani hiyo ya mwaka 2021 kwa Zanzibar na wamepatiwa mafunzo ya taratibu za usimamizi wa mitihani.

Mkurugenzi huyo aliwapongeza walimu wote kwa juhudi kubwa wanazochukua katika kuwalea watoto kitaaluma na kimaadili mema na kuwatakaa wazazi, walezi na wananchi wote kuwa karibu zaidi na watoto wao wanaofanya mitihani hiyo na wahakikishe kuwa wanafika katika vituo vyao vya mitihani kwa wakati kwa ajili ya kutumia haki yao ya msingi ya elimu.

“Baraza la Mitihani linapenda kuweka wazi kwamba, ufanyaji wa mtihani unahitaji amani na utulivu wa hali ya juu, hivyo linawasihi kwamba mtu yeyote asiyehusika asijaribu kusogelea kituo cha mtihani, kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria na kanuni za mitihani, na kwa yeyote atakayepatikana na hatia, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake,” alisema.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, aliwataka watahiniwa wote kujiepusha na vitendo vyote vinavyokwenda kinyume na kanuni za mitihani ikiwamo kufanya udanganyifu, na atakayebainika kwenda kinyume na kanuni na taratibu za mitihani, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwamo kufutiwa kwa matokeo yake yote.



Katibu wa Taasisi ya Zanzibar ya Outreach Program (ZOP), Dk. Naufal Kassim (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu harambee ya uchangiaji wa hospitali ya kijamii. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Mwinyi awakaribisha wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewakaribisha wawekezaji na kampeni mbalimbali kuwekeza Zanzibar, huku akiwahakikishia mazingira bora ya uwekezaji.

Aliyasema hayo juzi katika hotuba yake iliyosomwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdula, katika maonyesho yalioandaliwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi yaliofanyika Zanzibar.

Alizitaka taasisi za kifedha pamoja na wadau wengine kuchangamkia fursa ya kujenga nyumba za makazi na kuondoa hofu juu ya uwekezaji huo kutokana na uhitaji mkubwa wa wananchi katika suala la makazi. “Nawaomba wawekezaji ondosheni hofu na wala musiwe na wasiwasi kwani uhitaji wa nyumba Zanzibar ni mkubwa,” alisema.

Katika hotuba hiyo ya Rais, Hemed alieleza kuwa serikali ya awamu ya nane inaendelea na mchakato wa kuipanga Zanzibar kwa kuanzisha miji mipya itakayojengwa nyumba za kisasa ikiwamo Matemwe, Chumbuni na Kilimani kwa upande wa Unguja na kwa Pemba ni Finya na Mfikiwa kwa ajili ya kuanzisha miji mipya.

Katika suala la uwekezaji alisema serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imeshatayarisha ma eneo ya Dunga na Pangatupu kama maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Alieleza kuwa, Zanzibar ikiwa nchi ya visiwa ina eneo dogo kijiografia hivyo, amewaelekeza wataalamu wa Wizara ya Aridh na Maendeleo ya Makazi kuendelea kuipanga ardhi yake kwa kuzingatia sera ya mipango miji.

Hata hivyo, aliipongeza wizara kwa ubunifu wao katika kufanikisha maonyesho hayo muhimu na ameuagiza uongozi wa Wizara hiyo kuyaendeleza maonyesho kila mwaka.

Naye Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Riziki Pembe Juma, alisema kwamba kufanyika kwa maonyesho hayo kunalenga kuunga mkono dhana ya uchumi wa bluu ambayo ina dhamiria kuinua hali ya uchumi wa Zanzibar pamoja na hali za wananchi wake.

# Taasisi kuchangisha fedha ujenzi hospitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya kuhudumia matibabu ya afya vijijini (Zanzibar Outreach Program ZOP) inatarajia kufanya harambee ya uchangishaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ambayo itasaidia kutoa huduma za afya kwa wananchi hasa wanyonge.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu wa taasisi hiyo, Dk. Naufal Kassim Muhamed, alisema kuwa taasisi hiyo ina lengo la kujenga hospitali hiyo baada ya kubaini kuwa wananchi wengi wanasumbuliwa na magonjwa mbalimbali, lakini wanakosa huduma za matibabu.

Alisema kuwa taasisi hiyo imekuwa na utaratibu wa kuwafikia wananchi vijijini kutoa huduma za afya kwa kuchunguza afya zao, lakini kilichogundulika ni kuwa wananchi wengi wamekuwa na wasiwasi baada ya kugundulika kuwa na mgonjwa sugu kama saratani ya matiti.

Alieleza kuwa baadhi ya wananchi huwasumbuliwa na magonjwa mbalimbali, lakini huwa hawajijui na hugundulika baada ya kupimwa afya zao.

Alieleza kuwa wanapoenda vijijini kutoa huduma za afya wamegundua kuwa ugonjwa wa saratani ya matiti umekuwa ukijitokeza kila eneo ambapo wanawake wa rika tofauti waliofanyiwa uchunguzi baadhi yao wamegundulika kuwa na tatizo hilo.

“Saratani ya matiti haina rika maalum, maana tumempata msichana mwenye umri wa miaka 13 ana tatizo la saratani ya matiti, hivyo niwaombe wananchi kuwa na utamaduni wa kuchunguza afya zao mara kwa mara,” alisema.

Alieleza kuwa pia wamegundua kuwapo kwa tatizo la usikivu kwa watoto ambapo wanapotoa elimu shuleni wamegundua wanafunzi wengi wanatokwa na usaha masikioni.

Aliwataka wazazi na walezi kuwa na utamaduni wa kuwachunguza watoto wao wanapowazaa ili kujua kama wana tatizo la usikivu na kupata huduma mapema.

Daktari huyo aliwataka wananchi kutumia vyakula vya asili ambavyo vinasaidia kinga nzuri ya afya mwilini kuliko kutumia vyakula vyenye kemikali ambavyo husababisha maradhi mbalimbali ikiwamo saratani.

# Mkenda asisitiza matumizi mbegu bora

**Na Pascal Mayalla**

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda (pichani), ameipongeza Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu TOSCI, kwa kazi nzuri, iliyopelekea Banda la TOSCI, kushinda tuzo ya banda bora.

Amewasisitiza wakulima wote wa Tanzania, kutumia mbegu zenye alama ya TOSCI ambazo ndizo mbegu zilizothibitishwa kutumika nchini.

Waziri Mkenda, alizitoa pongezi hizo katika mahojiano, baada kilele cha maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, zilifanyika kwenye viwanja vya Pasua, nje kidogo ya mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Waziri Prof. Mkenda alisema TOSCI imefanya kazi nzuri ya kurahisisha uhakiki wa mbegu kwa wakulima kwa kutumia njia za kisasa za kielektroniki, kuhakiki mbegu, kwa kutumia simu ya mkono, hivyo kuliwezesha Taifa kutumia mbegu zenye ubora uliothibitishwa na TOSCI, na pia kuisifu TOSCI kuyatumie maonyesho hayo kutoa elimu kwa umma, sio tuu kwa wananchi waliofika viwanjani, bali pia banda la TOSCI, limetoa elimu kubwa kupitia vipindi vya redio na TV vya Banda la TOSCI.

Prof. Mkenda alisema serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, imepania kufanya mapinduzi ya kweli ya kilimo, na kutoa umuhimu wa pekee kwa utafiti, ambapo bajeti ya utafiti imeongezwa maradufu, ambapo kwa kuanzia, itatumia sehemu ya Sh. bilioni 8 zilizotolewa na IFAD kwa serikali ya Tanzania, kwa kuzielekeza kwenye utafiti.



Akizungumzia umuhimu wa utafiti, Prof. Mkenda alisema: “ Naamini huko tunakowenda, utafiti ni suala muhimu sana kwenye kilimo kuliko ambavyo tumeweza kuamini huko zamani, ili tuweze kuendana na mbadiliko ya tabianchi, tuweze kuendana na mazingira yetu, ili kuendana na aina ya udogo, na afya ya udongo tunaotumia, lazima tufanye utafiti.”

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngediagi, alisema ushindi ni faraja kwa TOSCI nzima, menejimenti na wafanyakazi wote wa TOSCI ambao wanajituma kwa bidii na unazidi kuwapa ari ya kuendelea kujituma, kuwatumikia Watanzania.



Wafanyabiashara wakiwa katika kongamano la kibiashara lililoandaliwa na Benki ya KCB Tanzania linalofahamika Biashara Club, jijini Mwanza, ambapo wafanyabiashara walipata semina elekezi kutoka kwa viongozi, wafanyakazi na wadau wa benki hiyo kuhusu njia na mbinu zinazoweza kuongeza ufanisi katika biashara zao. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kirikuu NMB Bonge la Mpango zaenda Mbalizi na Mpanda

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wawili wametangazwa baada ya kushinda pikipiki za miguu mitatu aina ya Sky Mark kwenye awamu ya pili ya kampeni ya Weka Akiba na Ushinde inayoendeshwa na Benki ya NMB ‘NMB Bonge la Mpango - 2merudi Tena’.

Washindi hao ni Melkiadi Kepa wa Usongwe mkoani Mbeya na Anthony Meshack wa Mpanda mkoani Rukwa, NMB Bonge la Mpango ni kampeni itakayoendeshwa kwa wiki 12, ikilenga kuhamasisha utamaduni chanya wa kujiwekea akiba, ambako washindi 50 watajinyakulia pikipiki za mizigo 50 zenye thamani ya Sh. milioni 225, huku washindi 120 wakitarajia kujishindia fedha taslimu Sh. milioni 12.

Droo hiyo ilifanyika Ofisi za NMB Tawi la Magomeni mkoani Dar es Salaam, ambako Melkiadi wa NMB Tawi la Mbalizi Road na Anthony wa Tawi la Mpanda, ni kati ya washindi 12, ambako 10 miongoni mwao walishinda fedha taslimu Sh. 100,000 kila mmoja. Pikipiki mbili za Sky Mark ina thamani ya Sh. milioni 4.5.

Akizungumza kabla ya kuchezeshwa kwa droo hiyo, Meneja wa NMB, Tawi la Magomeni, Mary Marungi, alisema NMB Bonge la Mpango ni kampeni ya kimkakati, inayolenga kuhamasisha utamaduni chanya wa kutumia huduma za kibenki kwa kuweka ili kuwezesha utimilifu wa malengo ya mtu mmoja mmoja, kikundi ama taasisi.

“Kampeni hii ilizinduliwa Oktoba mwanzoni na itadumu Desemba, ambako kila wiki tutakuwa tukiwazawadia washindi 12, kati yao 10 watashinda fedha taslimu na wawili wanajinyakulia pikipiki za miguu mitatu aina ya Sky Mark zenye thamani ya Sh. milioni 4.5 kila moja.

“Ili kushindania zawadi hizo, mteja mwenye akaunti anapaswa kuweka akiba isiyopungua Sh. 100,000 na yule ambaye hana akaunti, anatakiwa kufungua na kuweka akiba isiyokuwa chini ya kiasi hicho na moja kwa moja atangia katika droo zetu hizi za kila wiki.

“Wito wetu kwao ni kuwataka waendelee kuweka akiba, ambapo licha ya kuwa njia ya kuwawezesha kufanikisha malengo yao, pia itawapa nafasi ya kujishindia zawadi hizi muhimu, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa mwaka na mwanzo wa mwaka ujao, ambako kunakuwa na sikukuu na pia malipo mbalimbali ya ada za watoto shuleni,” alisema Marungi.

Droo hiyo ilichezeshwa mbele ya Pendo Albert Mfuru, ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), aliyesema jukumu lake katika tukio hilo ni kuhakikisha vigezo na masharti yanayosimamia michezo hiyo vinafuatwa, huku akiwahakikishia wateja wa NMB kuwa bahati nasibu hiyo inaendeshwa kihalali na washindi wake wanapatikana bila upendeleo wowote.

Washindi 10 walioibuka na zawadi ya fedha taslimu katika droo hiyo ni Keneth Mkumbo, Hadija Abbi, Rose Nungu, Nesha Mlaki, Selina Mwalugaja, Mwanahamisi Mwingira, Ado Mbunda, Dismas Simsonga, Emmanuel Kirenga na Shabani Kalinga.

# Pinda ahamasisha wasomi kuchangamkia fursa kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewataka wasomi kuchangamkia fursa za kilimo kwa kuwa cheti cha shahada bila fedha hakina tija.

Pinda aliyasema hayo jana jijini hapa katika maadhimisho ya miaka mitano ya kampuni ya JATU PLC inayohusika na masuala ya kilimo.

Alisema msomi kulima akiwa na elimu yake sio mjinga bali ni mjanja wa kucheza na fursa.

“Mtu una cheti cha degree (shahada) halafu huna pesa ni sawa na kazi bure, jamii inapaswa kujiongeza badala ya kutegemea elimu peke yake, suala la degree ni makaratasi tu hayana maana kama hutayafanyia kazi ili upate fedha.”

“Vijana changamkieni fursa za kilimo kuna pesa ndani yake usibweteke na elimu peke yake,” alisema Pinda.

Alisema msomi akiendesha kilimo ni lazima atafanya kiutaalamu na kuwa mfano kwa jamii inayokuzunguka katika maeneo mbalimbali.

Alihimiza serikali kufungua milango kwa vijana ili kuwasilisha masuala ya kilimo katika Baraza la Mawaziri yafanyiwe kazi.

Alisema wakifanya hivyo watakuwa wamewasaidia kwa kiasi kikubwa vijana michango yao kutambulika na serikali.

Naye Mkurugenzi wa JATU, Peter Isaya, alisema taasisi hiyo inatambulika kimataifa na wao kila siku hufikiria kusonga mbele katika masuala ya kilimo.

Alisema watu wanapaswa kuwekeza hisa ili kupata mikopo ambayo itawasaidia kuendesha shughuli zao za kila siku.

Kadhalika, wanatarajia kuanzisha benki itakayokuwa ikijihusisha na mikopo ya kilimo kwa wakulima wawekezaji. Aliishukuru serikali kwa kuahidi kuwasaidia ili kufikia malengo yanayokusudiwa ya kuwanufaisha wakulima.

**HABARI KITAIFA**

# Taasisi yatoa msaada chakula kwa yatima

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIKA kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani, Taasisi ya Huduma za Kijamii ya Medewell kwa kushirikiana na Beta Charitable Trust imetoa msaada wa chakula kwa wajane na yatima 220 vyenye thamani ya shilingi milioni saba.

Akiongea wakati wa kukabidhi msaada huo, Ofisa Rasilimali watu wa Medewell, Amina Ramadhani, alisema taasisi hiyo inayomiliki kituo cha huduma za afya kwa gharama nafuu mwaka huu imeamua kukumbuka makundi hayo.

Amina alisema kila mwaka wanaadhimisha siku hiyo kwa kutoa chakula kwa watu wote bila kujali makundi na mwaka huu wamefanikiwa kuwakumbuka wajane na yatima.

Alisema Kituo cha Afya Medewell kimekuwa kikitoa huduma ya macho kwa gharama nafuu ili kuwezesha wananchi wenye kipato tofauti kumudu gharama, kupata matibabu na kuokoa afya zao.

Mdhamini wa Medewell, Haji Saheb, alisema chakula hicho kimetolewa kwa wajane na yatima bila kujali dini zao. Aliwataka wananchi kujenga tabia ya kusaidiana na kushirikiana na serikali katika utatuzi wa kero mbalimbali kwenye maeneo yao.

Alisisitiza suala la wazazi kusomea masuala ya dini wanazoabudu ili kuwalea watoto wao katika njia sahihi yenye hofu ya Mungu na maadili mema.

"Tusomeshe na watoto wetu wapate elimu ya dini zetu ili kupunguza ongezeka la wanawake wanaotelekezwa na watoto huku wakiwa hawana msaada kutoka kwa waume zao ambao wamekosa hofu ya Mungu," alisema.

Diwani wa Tumbi, Raymond Chokala, aliipongeza taasisi hiyo kwa kukumbuka makundi hayo kwenye jamii.

Naye muuguzi wa Kituo cha Afya Medewell, Hamida Fazal, alimwomba diwani kushirikiana na serikali kufanya ukarabati wa barabara kutoka kituoni hapo hadi barabara kuu.

# Jokate awaonyesha wanawake fursa elimu manunuzi ya umma

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wajasiriamali wamehimizwa kuzingatia elimu ya sheria ya ununuzi wa umma na matumizi ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki (TANePS), yanayotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) ili kushiriki kikamilifu katika fursa za zabuni za umma na kujikwamua kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, ndiye aliyetoa ametoa hamasa hiyo alipokuwa akifungua mafunzo ya sheria ya ununuzi kwa wanawake mkoani Dar es Salaam, akimwakilisha Katibu Tawala wa Mkoa huo.

Jokate alisema anaamini baada ya mafunzo hayo yaliyohudhuriwa na zaidi ya wanawake wajasiriamali 100 wa mkoa huo, watakuwa na uwezo wa kuandaa nyaraka za zabuni zenye ubora na zinazokidhi vigezo vyote ili wapate fursa za zabuni za umma na kujikwamua kiuchumi.

Aidha, alisema mafunzo hayo yamefanyika wakati sahihi kwa kuwa serikali imetangaza miradi mingi zaidi hivi karibuni, ambayo ni fursa inayopaswa kuchangamkiwa na wanawake pia.

Alieleza kuwa hivi sasa serikali kupitia PPRA inahakikisha michakato ya zabuni inafanywa kwa uwazi na usawa kupitia TANePS ili kupata thamani ya fedha, hivyo, aliipongeza PPRA kwa kuwapa wanawake hao mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo huo.

"Sasa hivi kuna fedha nyingi ambazo Rais Samia Suluhu Hassan ametoa kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwamo ya ujenzi wa madarasa kwa ujumla zaidi ya 18,000, kuna ujenzi wa zahanati na mengine.

"Hizi fursa zote zinaingia kwenye Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS). Mimi naamini fursa zipo, cha muhimu ni uelewa au ufahamu wa jinsi ya kuzipata. Ninaipongeza PPRA inatoa elimu hiyo," alisema Jokate.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Mhandisi Mary Swai, alisema mamlaka hiyo imeanza na wanawake kwa kuwa imeona ingawa wana nia ya kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali, bado katika ushiriki wa zabuni za umma idadi ya wanawake ni ndogo ukilinganisha na wanaume.

Mhandisi Swai alisema mamlaka inatoa mafunzo kwa makundi yote na kwamba siku chache zilizopita ilitoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi), na ina mpango wa kuwafikia vijana na wazee.

"Ni jukumu letu kuhakikisha wanakuwa na uelewa wa kushiriki kikamilifu michakato ya ununuzi wa umma. Mwezi uliopita tulifundisha watu wenye ulemavu wa kusikia mkoani Morogoro. Tunapanga kuwafundisha vijana na wazee ili wote wachangamkie hii asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi inayotengwa na taasisi nunuzi kwa matakwa ya sheria," alisema Mhandisi Swai.

Wakizungumza baada ya mafunzo hayo, washiriki waliipongeza PPRA kwa kuwapa uelewa na serikali kwa kwa kutoa fursa za zabuni.

"Elimu niliyoipata itanisaidia kwa vitu vingi, itanisaidia kuandaa nyaraka za zabuni na hata kutumia TANePS kuziwasilisha. Tukipata tenda za serikali tutajikwamua zaidi kiuchumi," alisema Happy Kisamo, mmoja kati ya washiriki wa mafunzo hayo.

Sheria ya Ununuzi wa Umma inazitaka taasisi nunuzi kuhakikisha kuwa zinatenga asilimia 30 ya bajeti yake ya ununuzi kwa ajili ya makundi maalum ambayo ni wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.



Mgeni rasmi kwenye mahafali ya Shule ya Awali ya St Anne Marie Academy, Joyce Chamuhuo, ambaye ni mkuza mitaala wa Taasisi ya Elimu (TIE), akimkabidhi cheti mmoja wa wanafunzi waliomaliza elimu ya awali shuleni hapo, yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kahama yapokea bil. 1.9/- kujenga madarasa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imepokea Sh. bilioni 1.9 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 95 katika shule za sekondari 19.

Kati ya fedha hizo Sh. milioni 40 zitajenga vyumba vya madarasa katika shule shikizi za Ngugu na Mbulu huku Sh. milioni 160 zikielekezwa kujengwa mabweni mawili shule za msingi zenye mahitaji maalumu kata ya Mwime.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Yahaya Bundala, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Alisema kila shule ya sekondari imepewa mgao wa fedha hizo kulingana na mahitaji yake ya madarasa.

Pia, wamepokea Sh. bilioni 1.9 za kutatua uhaba wa madarasa kwa shule za sekondari 19 ili kuhakikisha ifikapo mwakani wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanapata nafasi ya kukaa na kosoma.

Aidha, Yahaya alizitaja sekondari hizo na namba zilizopo kwa kwenye mabano na idadi ya madarasa kuwa ni Seeke (6) milioni 120, Kabela Gold (5) milioni 100, Isunuka (3) Sh. milioni 60, Nyandekwa (4) Sh. milioni 80, Ngogwa (5) Sh. milioni 100, Mwendakulima (4) Sh. milioni 80, Bugisha (4) Sh. milioni 80, Nyihogo (11) Sh. milioni 220, Nyasubi (6) Sh. milioni 120.

Sekondari nyingine ni Kishimba (3) Sh. milioni 60, Mama Samia (9) Sh. milioni 180, Kinaga Sh. milioni 100, Bukamba Sh. milioni 80, Iyenye Sh. milioni 100, Mpera Sh. milioni 60, Isagehe Sh. milioni 120, Kitwana Sh. milioni 100 pamoja na sekondari ya Abdul Rahim Busoka Sh. milioni 40.

Naye Mkurugenzi wa manispaa hiyo, Anderson Msumba alisema, licha ya kupokea fedha hizo bado wanachangamoto ya uhaba wa madarasa 153 katika shule za msingi na kwamba wanaendelea kutatua matatizo mbalimbali kwa kushirikiana na wananchi.

Alisema halmashauri imetenga Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika shule za msingi na Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kuanzia msingi hadi kuweka samani za ndani.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Mhungula, Scolastica Bebete alisema atahakikisha Sh. milioni 220 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 11 Shule ya Sekondari Nyihogo, inatumika katika matumizi yaliyopangwa na wanafunzi wanapata sehemu nzuri ya kusomea.

# SHIRATI MJI, WANAMAJI SASA TAMBO ZATAWALA UMOJA CUP

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kushika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Kundi D linaloongozwa na Kirengo FC, katika michuano ya Umoja Cup 2021, inayoendelea wilayani Rorya mkoa wa Mara, mabingwa watetezi wa mashindano hayo ambayo hufanyika kila mwaka, timu ya Shirati Mji FC, wamesema kama ilivyokuwa mwaka jana wakati wakijulikana kwa jina la Town Stars, hawatakubali ubingwa huo utoweke mikononi mwao.

**Michuano hiyo inayodhaminiwa na mdau wa michezo wilayani Rorya, Peter Owino (Jasota) Ochieng, kwa mwaka wa tisa sasa, na mwaka huu ikibeba jina la mchezaji wa Wanamaji fc, Makori Odoyo maarufu (Abega wa Cameroon), inakaribia kumaliza raundi ya kwanza.**

Kabla ya mechi za jana, Kundi A lilikuwa linaongozwa na timu ya Mennonite FC ikifuatiwa na Magamaga fc, huku Kundi B Rifa fc ikiwa kileleni ikifuatiwa na Watumishi fc na Kundi C likiongozwa na wenyeji wa mashindano hayo, Wanamaji FC wakifuatiwa na Vijana wa Masonga fc.

Uongozi wa Shirati Mji FC, ulimwambia mwandishi wetu kuwa Kombe la Umoja Cup mwaka huu ni la kwao tena na kwamba wamefurahi kuona timu nyingi zimejitokeza kuwasindikiza kuchukua ubingwa huo kwa mara nyingine na wanachokizingatia ni kuwaheshimu wapinzani wao kama timu lakini si kuwaachia taji hilo.

Wakati Shirati Mji FC, wakitoa tambo hizo, Kiungo wa Wanamaji fc, ambao ndio wenyeji wa mashindano hayo, Tumaini Nelson 'Tuma', alisema hawatakubali kuona kombe hilo linaondoka tena nyumbani na wao kubaki kama wasindikizaji.

"Hili kombe la mwaka huu limepewa jina la mchezaji wetu wa zamani aliyefariki hivi karibuni, hivyo tunatamani tulinde heshima kwa kulibakiza nyumbani. Tunajua mashindano mwaka huu ni magumu, lakini ili kushinda ligi yoyote huwa inabidi kupambana na timu ngumu, hivyo tumejiandaa kwa hilo, na uzuri ni kwamba tuko nyumbani, hatutapenda kuwaangusha mashabiki wetu na hatutapenda kuiangusha familia ya Abega," alisema Tuma.

Alisema pia ni fahari kwao kumpa heshima mdhamini wa mashindano hayo, Owino, ambaye ni mwenyeji wa eneo hilo, na kwamba wamejipanga kucheza kufa au kupona ili kulibakisha kombe hilo nyumbani.

Fainali ya michuano hiyo inayoshirikisha timu 20 zikiwa katika makundi manne yenye timu nne kila kundi, inatarajiwa kupigwa Desemba mwaka huu pamoja na ile ya mchezo wa pete ambayo pia inadhaminiwa na Owino.

Katika hatua nyingine, Meneja wa Umoja Cup, Obong'o Maina, amesema timu ya Rifa fc ya Michire, imefanikiwa kulipa faini aliyotozwa mchezaji wao, Ouma Kiraryo baada kufanya fujo katika fainali ya Umoja Cup 2020 ambapo Kamati ya Maandalizi ya michuano hiyo ilimpa adhabu ya kukosa mechi tatu za mwaka huu na kulipa faini ya Sh. 10,000.

Obong'o pia alisema mchezaji mwingine wa Rifa fc, Gai Magatti, bado anaendelea kutumikia adhabu yake ya kutokushiriki mashindano ya mwaka huu baada ya kushiriki kumfanyia fujo mwamuzi wa mechi ya fainali mwaka jana.



Kikosi cha mabingwa watetezi michuano ya Umoja Cup inayoendelea wilayani Rorya, Shirati Mji fc. **NA MPIGACHA WETU**

## Sekta ya Ujenzi yaichapa Mambo ya Nje SHIMIWI

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), wameibuka washindi katika mashindano ya michezo ya Idara na Wizara za Serikali (SHIMIWI) kwenye mchezo wa pete kwa kuwafunga wenzao wa Wizara ya Mambo ya Nje.

Mashindano hayo yalifanyika mkoani Morogoro, mgeni rasmi akiwa ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, na katika mchezo huo walishinda kwa mabao 21 dhidi ya 14 ya wapinzani wao.

Akizungumza katika ufunguzi huo, Makamu wa Rais, Dk. Mipango, aliwataka wachezaji kuwa na umoja kati ya wizara, taasisi moja na nyingine na kutaka mchezo uchezwe kwa kufuata nidhamu na maadili ya kiutumishi.

Aidha, Dk. Mipango alizitaka taasisi na wizara kufanya mazoezi angalau kwa wiki mara moja kwa watumishi wote kwa muda muafaka bila kuharibu ratiba ya kazi.

Pia, alizipongeza baadhi ya wizara na taasisi zote ambazo zina utaratibu wa kufanya mazoezi kuendelea na mazoezi hayo.

Aidha, aliwapongeza waajiri wote wa taasisi na wizara kwa kuwaruhusu watumishi kwenda kushiriki kwenye mashindano hayo.

Katika michezo mingine, wafanyakazi wa ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ( TAMISEMI), waliibuka kidedea kwa kuwachapa wafanyakazi wa ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mara mabao 50-4 katika mchezo wa pete.

Wafanyakazi wa sekta ya ujenzi, leo wanacheza na wenzao wa Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mara, kwenye mchezo wa pete, huku katika mchezo wa kuvuta kamba ukiwakutanisha wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Nje dhidi ya wenzao wa Wizara ya Mambo ya Ndani.

# St. Anne Marie kuibua na kuendeleza vipaji

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya St. Anne Marie Academy, imeweka mpango kabambe wa kuibua na kuendeleza vipaji vya wanafunzi katika michezo mbalimbali na sanaa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Jasson Rweikiza kwenye mahafali ya 19 ya shule hiyo yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule hiyo, Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam.

Alisema mbali na kuendelea kufanya vizuri kitaaluma, wameona ni vema wakaanzisha mpango huo ili kuwaibua wanafunzi wenye vipaji mbalimbali kama kuimba, kukimbia, kucheza mpira na vipaji vingine ambavyo wanafunzi wengi wa shule hiyo wameonyesha kuwa navyo.

"Mwanafunzi anaweza kuwa wa kawaida kwenye masomo, lakini akawa na kipaji ambacho iwapo kitaibuliwa na kuendelezwa, anaweza kufika mbali sana, tunaweza kupata waimbaji wa kimataifa," alisema Rweikiza ambaye ni Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM).

Alisema mpango mwingine wa shule hiyo ni kuhakikisha inashika nafasi ya kwanza kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba kwani uwezo huo wanao kutokana na rekodi nzuri waliyonayo.

Alisema shule hiyo imekuwa ikiingia kwenye shule 10 bora kitaifa kwa miaka mingi na wanafunzi wake kuingia kwenye 10 bora kitaifa hivyo hawaoni kikwazo cha shule hiyo kushika namba moja kitaifa.

Mgeni rasmi kwenye mahafali hayo, Joyce Chamuhuo, ambaye ni mkuza mitaala wa Taasisi ya Elimu (TIE), alisema kuna umuhimu kwa shule mbalimbali kutenga angalau siku mbili za kuibua vipaji vya wanafunzi kwenye nyanja mbalimbali na kuviendeleza.

Aliwataka wazazi nao kuwa na kawaida ya kuwafundisha lugha za makabila watoto wao ili kuendeleza tamaduni zao kwani baadhi yao hawajui hata kusalimia kwa kutumia lugha za nyumbani.

"Nimefurahi kusikia Mkurugenzi anasema wameweka mpango wa kuibua vipaji na kuvikuza, hili ni jambo zuri sana na nyinyi shule binafsi mnaliweza sana hili kwa sababu mna muda mrefu wa kukaa na wanafunzi hawa," alisema.

"Mkurugenzi amesema hapa kwamba mwanafunzi anaweza asiwe mzuri sana kwenye masomo, lakini akawa na kipaji cha kuimba au kucheza na kikiibuliwa na kuendelezwa kinaweza kumfikisha mbali tengeni muda wa kutekeleza jambo hili," alisema.

## ZISIKUPITE

### COADY ATAKIWA NEWCASTLE

NAHODHA wa Wolves, Conor Coady, 28, yupo kwenye orodha ya wanaowaniwa na Newcastle United katika uhamisho wa Januari, huku ikielezwa anaweza kuigharimu kiasi cha pauni milioni 20. ***(Sun)***

### POGBA KUBAKIZWA UNITED

MANCHESTER United watafanya kila wanachoweza kuhakikisha wanambakiza kiungo wao, Mfaransa Paul Pogba, 28, hapo Old Trafford huku Real Madrid wakitumaini kumsajili mchezaji huyo mwishoni mwa msimu huu. ***(AS)***

### PEPI AWANIWA EPL

STRAIKA kinda wa FC Dallas, Ricardo Pepi, anazivutia klabu za Ligi Kuu England (EPL), Liverpool, Manchester United, Brentford na Brighton. ***(Mirror)***

### OVERMARS ATAKA KAZI

WINGA wa zamani wa Uholanzi, Marc Overmars, amefungua mazungumzo na Newcastle United ili kuwa mkurugenzi wao mpya wa soka, nafasi ambayo anaitumikia kule Ajax. ***(Mirror)***

### SUAREZ ATAKA KUBAKI

STRAIKA wa Atletico Madrid na Uruguay, Luis Suarez, anataka kubaki klabuni hapo baada ya msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye amefunga mabao matano msimu huu, mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(Marca)***

### AMKANUSHIA TIELEMANS

KOCHA Brendan Rodgers amekanusha madai kwamba, kiungo wake wa kimataifa wa Ubelgiji, Youri Tielemans amekataa ofa ya kusaini mkataba mpya hapo Leicester City, huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, akihusishwa kuwaniwa na Liverpool na Manchester United. ***(Mail)***

### DYBALA KIMEELEWEKA JUVE

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Paulo Dybala, mwenye umri wa miaka 27, amefikia makubaliano ya mkataba mpya na Juventus. ***(Calciomercato)***

### YAONYWA KWA KOUNDE

CHELSEA imeonywa na Sevilla kwamba, klabu hiyo ya Hispania haitamuuza mlinzi wao nyota raia wa Ufaransa, Jules Kounde, 22. ***(Sun)***

### PEP AMTAKA KROOS

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anamfuatilia kwa karibu mlinzi wa Real Madrid, Toni Kroos, 31, raia wa Ujerumani ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2023. ***(El Nacional)***

### TORRES MKATABA MPYA

MANCHESTER City inajipanga kumpa mkataba mpya straika wa Hispania, Ferran Torres, 21, ambao utamfikisha mwaka 2027, huku mshahara wake ukiongezeka hadi pauni 100,000 kwa wiki. ***(Daily Star on Sunday)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH: NIPO TAYARI KUSTAAFIA LIVERPOOL

## Kama ukiniuliza mimi kuhusu mikataba, nitapenda kubaki hapa hadi siku ninastaafu, lakini...

**LIVERPOOL,** England

WAKATI ulimwengu wa soka ukiendelea kufuatilia ni nini kitatokea kwa Mohamed Salah wakati mkataba wake unaelekea ukingoni, yeye mwenyewe amesafisha hali ya hewa kuhusu majaliwa yake.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumapili ambao Liverpool ilikuwa ikicheza na wapinzani wao wakuu kwenye Ligi Kuu England, Manchester United, Salah alionyesha nia ya kutaka kubakia kwenye dimba hilo la Anfield.

Salah amesema kwamba, malengo yake ni kumalizia soka lake hapo Liverpool, lakini yeye si mwamuzi wa mwisho kuhusu hilo.

**"Kama ukiniuliza mimi (kuhusu mikataba), nitapenda kubaki Liverpool hadi siku ninastaafu soka, lakini siwezi kulizungumzia sana hilo, halipo mikononi mwangu," alisema Salah akinukuliwa na Sky Sport.**

"Inategemea na klabu inataka nini, si (mimi) ninataka nini. Kwa sasa, sijioni nikicheza dhidi ya Liverpool, lakini tutaona nini kitatokea baadaye."

Kwa siku za karibuni, Liverpool wamemalizana na habari za mikataba mipya kwa baadhi ya wachezaji muhimu kwenye kikosi chao.

Kinachofikirisha ni mkataba wa Salah ambaye amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake lakini, hadi sasa hakijaeleweka.

Mapema hivi karibuni ESPN ilimnukuu wakala wake akisema kwamba, Salah anataka kuongezewa mshahara hadi pauni 400,000 kwa wiki ili aweze kukubali kusaini mkataba mpya na 'Wekundu' hao.

Hadi sasa Salah ameshapachika mabao 12 katika michezo 11 aliyoitumikia Liverpool msimu huu kwenye michuano yote, kabla ya mechi ya jana Jumapili dhidi ya Man City.

MECHI KALI
HOME
AWAY
BESIKTAS
2.36 | 3.36 | 2.82
GALATASARAY
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# Ni Simbu Rock City Marathon 2021, Watanzania wang'ara




Naibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (wapili kuli), akimvisha medali mshindi wa kwanza wa mbio za KM. 21 za Rock City Marathon, Mwanariadha Alphonce Simbu, baada ya kutumia muda wa saa 01:06:19 kwenye mbio hizo zilizofanyika jijini Mwanza jana. Wanaoshuhudia ni pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala (kulia) na Rais wa Shirikisho la Riadha Taifa, Silas Isangi. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Mwandishi Wetu**

MWANARIADHA wa kimataifa kutoka Tanzania, Alphonce Simbu, ameibuka mshindi wa kwanza kwenye mbio za KM. 21 za Rock City Marathon 2021, zilizofanyika jana jijini Mwanza baada ya kumaliza kwa muda wa saa 01:06:19, akifuatiwa na mshiriki kutoka nchini Kenya, Benard Musau aliyetumia muda wa saa 01:07:06.

Katika mbio hizo pia zilishuhudiwa Mtanzania mwingine, Shingade Giniki akimaliza katika nafasi ya tatu baada ya kutumia muda wa saa 01:07:35

Mbio hizo za kilomita 21 zilianzia viunga vya Jengo la Rock City Mall jijini humo kupitia mitaa mbalimbali ya jiji hilo ikiwamo mzunguko wa samaki na kumalizikia kwenye viunga hivyo huku zikipambwa na uwapo wa Naibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja sambamba na ushiriki wa watoto wadogo kuanzia umri wa miaka mitano walioshiriki mbio za Km. 2.5 zilizofahamika kama Uniliver Rock City Junior Challenge pamoja na watu wenye ulemavu wa ngozi yaani Albino walioshiriki mbio za Km. 5.

Upande wa wanawake mshindi wa kwanza katika mbio za Km. 21 ni Mkenya Isgani Chameo, aliyetumia muda wa saa 01:17:31 akifuatiwa na Watanzania Neema Msuhadi na Tunu Endrew, waliotumia muda wa saa 01:23:06 na 01:25:17

Washindi wa kwanza kwa jinsia zote katika mbio hizo zilizofanyika kwa mara ya 12 jijini Mwanza, waliibuka na kitita cha Sh. milioni mbili kila mmoja, washindi wa pili Sh. milioni 1.3 na washindi watatu Sh. 700,000.

Akizungumzia siri ya ushindi wake, Simbu alisema chachu ya mafanikio hayo ni kujituma kwake zaidi katika kufanya mazoezi kwa ajili ya mashindano hususan ya kimataifa na kwamba amekuwa na desturi ya kujiandaa vema kila mbio anazoshiriki.

"Kwangu mimi huwa najiandaa vema kwa kila mbio ninazoshiriki iwe za ndani au nje ya nchi kwa kuwa naamini ili niweze kufanya vizuri, mbio za kimataifa, lazima nianzie kufanya vizuri mbio za ndani. Niwashukuru waandaaji wa mbio hizi kwa maandalizi mazuri na niwaombe wadau waendelee kuwaunga mkono ili waendelee kuziboresha zaidi," alisema Simbu.

Mashindano hayo ya kila mwaka yaliandaliwa na Kampuni ya Capital Plus kwa udhamini wa Kampuni za Tiper, Benki ya KCB, Kampuni ya Magare, Kampuni ya Unilever sambamba na wadau wengine wakiwamo Hospitali ya Bugando, CF Hospital, Garda World, Maji ya Uhai, Serengeti, NSSF, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Rock City Mall, Pepsi na Chuo cha SAUT.

Mbali na Km. 21, mbio hizo pia zilihusisha Km. 10 zilizofahamika kama KCB Bank Rock City Corporate Challenge, mbio za Km. 5 zilizofahamika kama Magare Rock City Fun Run pamoja na mbio za Km 2.5 kwa ajili ya watoto zilizofahamika kama Uniliver Rock City Juniour Challenge.

Akizungumza baada ya kukabidhi zawadi kwa washindi na washiriki wa mbio hizo, Naibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Masanja alisema pamoja na kutangaza utalii mbio hizo ni nyenzo muhimu ya kuwaandaa wanariadha nchini kuwa katika nafasi ya kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa na kuirudishia nchi heshima yake katika mchezo huo.

"Serikali tunaahidi kuendelea kuunga mkono mbio hizi ili ziweze kuendelea kututangaza ndani na nje ya nchi," alisema Masanja huku akiahidi kudhamini safari ya washindi wa mbio hizo ili waweze kutembelea hifadhi ya Taifa ya Saanane kujionea vivutio vya utalii katika hifadhi hiyo ikiwa ni hatua ya kuunga mkono kaulimbiu ya mbio hizo ya kutangaza utalii kupitia michezo.

Mratibu wa Mbio hizo, Kasara Naftal alisema mbio hizo zimeweza kufanyika kwa mafanikio makubwa na ushirikiano walioupata kutoka uongozi wa mkoa wa Mwanza, Shirikisho la Riadha Taifa, Chama cha Riadha Mkoa wa Mwanza (MWAAA), Jeshi la Polisi mkoa wa Mwanza huku pongezi pia zikielekezwa kwa wadhamini wa mbio hizo kwa kuzifanikisha.

LIVE IN PLAY



# EVRA AFUNGUKA MWALIMU KUMNYANYASA KINGONO

**LONDON,** England

MLINZI wa zamani wa Manchester United, Patrice Evra, amesema alinyanyaswa kingono na mwalimu wake alipokuwa katika umri wa kupevuka (balehe).

Evra, mwenye umri wa miaka 40, alizungumzia hilo wazi katika mahojiano na gazeti la The Times la Uingereza kabla ya kutoa kitabu chake, juzi.

Alielezea ni kwa nini hakuwahi kuzungumzia suala hilo hadi sasa.

"Kwanza nilipoandika kitabu, sikuelezea hadithi yote kwa sababu nilikuwa nina aibu na kuogopa ni nini watu wangefikiria," alisema Evra.

"Sasa ninataka kusema kwa sababu sitaki watoto wawe katika hali yangu na kuhisi kuaibika, wakifikiria kwamba hawana ujasiri, ni suala la utayari wa akili wa kuzungumzia suala hili.

"Kwa hiyo ninataka kuwafanya watoto wawe na ujasiri na wasijilaumu wenyewe, kwa sababu kila mara nimekuwa nikijilaumu mwenyewe.

"Sina aibu ya kusema kuwa nilihisi kama muoga kwa miaka mingi kwa sababu sikuwahi kuzungumzia unyanyasaji huu wazi. Kilikuwa ni kitu kizito kifuani mwangu. Lakini sikufanya mwenyewe. Ninafanya kwa ajili ya watoto wengine."

Evra, ambaye alikulia katika kitongoji cha Les Ulis karibu na Jiji la Paris nchini Ufaransa, amesema unyanyasaji huo dhidi yake ulifanyika katika nyumba ya mwalimu, ambako aliishi ili kupunguza muda wa usafiri baina ya nyumbani kwao na shuleni.

Alimwambia tu mama yake wiki mbili zilizopita, na akasema alikataa ombi la mama yake ambaye alimtaka asijadili jambo hilo katika kitabu.

"Ni sasa wakati nina umri wa miaka 40 ndio nimemwambia mama yangu," alisema. "Ulikuwa ni mshtuko mkubwa kwake. Alikasirika sana. Aliniambia pole. Alisema, 'Usiweke hili katika kitabu chako,




Mshindi wa Bonasi ya Jackpot, Salum Hamisi Kidile, kutoka Mwenge mkoani Singida, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 27.7 baada ya kushinda kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot ya SportPesa wiki hii imefika Sh. 595,659,980. **PICHA: SPORTPESA**

## *Lukaku, Werner nje mwezi mmoja*

**LONDON,** England

WASHAMBULIAJI wa Chelsea, Romelu Lukaku na Timo Werner wanategemewa kuwa nje ya uwanja kwa muda usiopungua wiki nne (mwezi mmoja).

Wachezaji hao waliumia wakati wa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Malmo, Jumatano iliyopita na klabu ya Chelsea imethibitisha kwamba, itawakosa kwa muda usiopungua mwezi mmoja.

Chelsea wanapitia ratiba ngumu kutokana na mashindano kuongezeka huku wakihitaji huduma za washambuliaji wao tegemeo ambao wameumia kwa pamoja.

Chelsea walianza kuwakosa wachezaji hao katika mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Norwich City uliopigwa Uwanja wa Stamford Bridge, Jumamosi wakati wakishinda mabao 7-0.

Pia nyota hao wanatarajia kukosa mchezo wa EFL dhidi ya Southampton kesho Jumanne na pia kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle mwishoni mwa wiki.





MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 25 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 3858 | FC Andijon vs Nasaf Qarshi | 8.32 | 4.55 | 1.32 |
| 15:30 | 1249 | MFK Dubnica vs FC Stk 1914 Samorin | 2.46 | 3.53 | 2.46 |
| 15:30 | 1999 | Concordia Chiajna vs FC Brasov Steagul Renaste | 1.54 | 3.86 | 5.41 |
| 16:00 | 4270 | Swansea U23 vs Watford U23 | 2.41 | 3.53 | 2.52 |
| 16:00 | 5770 | National Bank vs Talaea El Gaish | 2.71 | 2.96 | 2.71 |
| 16:15 | 1378 | CA Progreso vs IA Sud America | 1.92 | 3.34 | 3.64 |
| 17:20 | 1915 | Al-Shamal vs Lekhwiya SC | 9.68 | 6.58 | 1.19 |
| 17:20 | 4260 | Al Ahli Doha SC vs Al Arabi Doha SC | 4.25 | 3.72 | 1.69 |
| 17:30 | 4322 | Clinceni vs UTA Arad | 3.83 | 3.15 | 2.00 |
| 18:00 | 3274 | Santiago Morning vs Deportes Iquique | 2.47 | 3.10 | 2.72 |
| 18:00 | 5627 | Sabayil vs Karabakh | 7.55 | 4.55 | 1.35 |
| 18:30 | 2537 | Botev Plovdiv vs Ludogorets Razgrad | 5.04 | 4.26 | 1.51 |
| 18:30 | 4255 | Santiago Wanderers vs Antofagasta | 2.25 | 3.34 | 2.86 |
| 18:30 | 5428 | Smouha Club vs El Ittihad Alexandria | 2.18 | 3.19 | 3.29 |
| 19:00 | 3220 | Paeek vs Omonia Nicosia | 6.34 | 3.96 | 1.52 |
| 19:00 | 4190 | Stomil Olsztyn vs Sandecja | 2.82 | 3.25 | 2.31 |
| 19:00 | 4191 | Anorthosis Famagusta vs AEK Larnaca | 1.98 | 3.47 | 3.61 |
| 19:00 | 4494 | Lokomotiv Moscow vs Sochi | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 19:45 | 2885 | Cerro Largo FC vs Plaza Colonia CD | 2.62 | 3.15 | 2.52 |
| 19:45 | 3873 | Qatar SC vs AL Wakrah | 2.47 | 3.05 | 2.76 |
| 20:00 | 3683 | Odds BK 2 vs Kjelsaas | 3.43 | 3.63 | 1.89 |
| 20:00 | 4271 | Besiktas vs Galatasaray | 2.36 | 3.36 | 2.82 |
| 20:00 | 4316 | IFK Varnamo vs Falkenbergs | 1.79 | 3.65 | 4.40 |
| 20:00 | 4318 | Aalborg vs Viborg FF | 1.89 | 3.59 | 3.74 |
| 20:00 | 5504 | Duisburg vs Kaiserslautern | 3.10 | 3.44 | 2.14 |
| 20:00 | 5844 | Orebro SK vs Degerfors | 2.31 | 3.42 | 2.70 |
| 20:15 | 2089 | Maccabi Tel Aviv vs FC Ashdod | 1.37 | 4.46 | 7.17 |
| 20:30 | 1017 | CFR Cluj vs Sepsi Osk | 1.76 | 3.39 | 4.62 |
| 20:30 | 2108 | Aldosivi vs Arsenal Sarandi | 2.11 | 3.15 | 3.30 |
| 20:30 | 3388 | Hodd vs Valerenga IF 2 | 1.14 | 7.54 | 11.61 |
| 20:30 | 4912 | Sarmiento Junin vs NewellS Old Boys | 2.37 | 3.10 | 2.85 |
| 20:45 | 3254 | Maccabi Haifa vs Maccabi Netanya | 1.48 | 4.08 | 5.82 |
| 21:00 | 4343 | Pontedera vs AC Reggiana | 3.87 | 3.17 | 2.01 |
| 21:00 | 5345 | Gil Vicente vs Sporting Braga | 3.79 | 3.30 | 1.97 |
| 21:45 | 1724 | Larne vs Linfield Belfast | 2.75 | 3.43 | 2.27 |
| 21:45 | 1835 | Bohemians FC vs Waterford Utd | 1.40 | 4.26 | 6.77 |
| 21:45 | 2527 | Red Star vs Le Mans | 2.31 | 3.22 | 2.93 |
| 21:45 | 3215 | AJ Auxerre vs Bastia | 1.82 | 3.45 | 4.24 |
| 21:45 | 4367 | St Patricks vs Dundalk FC | 2.20 | 3.15 | 3.10 |
| 21:45 | 5066 | Bradford PA vs Blyth Spartans | 2.27 | 3.50 | 3.00 |
| 21:45 | 5659 | Chelmsford vs Dartford | 5.00 | 4.20 | 1.61 |
| 22:00 | 1448 | Getafe vs Celta Vigo | 2.60 | 2.96 | 3.01 |
| 22:00 | 1979 | CD Palestino vs La Serena | 1.64 | 3.78 | 4.55 |
| 22:00 | 4061 | Feralpisalo vs Padova | 3.08 | 2.98 | 2.44 |
| 22:00 | 4302 | Girona vs Zaragoza | 2.17 | 3.05 | 3.49 |
| 22:00 | 5535 | River Plate (URU) vs CA Fenix | 1.73 | 3.71 | 4.05 |
| 22:45 | 1209 | Atletico Tucuman vs Patronato Parana | 2.05 | 3.15 | 3.44 |
| 22:45 | 3963 | Lanus vs Talleres | 2.16 | 3.14 | 3.19 |
| 23:00 | 2306 | Club Cortulua vs Chico | 2.31 | 3.05 | 3.00 |
| 23:15 | 3652 | Boavista vs Belenenses | 1.97 | 3.21 | 3.90 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo


Jumatatu Oktoba 25, 2021

Nipashe






Salah: Nipo tayari kustaafia Liver UKURASA 21


Kiungo wa Simba, Rally Bwalya akiifungia Simba bao pekee wakati ikiangukia pua kwa mabao 3-1 dhidi ya Jwaneng Galaxy kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: SIMBA**

## Azam: CAF basi, akili kwa Yanga

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutolewa katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema akili na nguvu zote sasa wanazihamishia katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara ukiwamo ule wa Oktoba 30, mwaka huu dhidi ya Yanga.

Azam juzi ilitolewa katika michuano hiyo ya kimataifa kwa kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Pyramids ya Misri ikiwa ni baada ya kutoka suluhu katika mchezo wa kwanza nyumbani.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa simu, Vivier alisema wamepokea matokeo hayo na sasa wanarejea nyumbani kujipanga kwa michezo iliyopo mbele yao ikiwamo ya Ligi Kuu na Kombe la FA.

Alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa na baada ya kufungwa walilazimika kuanza kutafuta bao la kusawazisha, lakini hawakuwa na bahati, sasa nguvu wanazihamishia kwenye mchezo dhidi ya Yanga.

"Ulikuwa mchezo mzuri tulijitahidi kupambana kwa ajili ya kupata matokeo, lakini tumeshindwa kufikia malengo sasa tunarudi nyumbani kupambana katika ligi, tunahitaji, kupambana na kufanya vizuri mechi zetu za nyumbani," alisema Vivier.

Alisema baada ya kushindwa kufikia malengo yao ya kucheza hatua ya makundi ya CAF, sasa wanarejea kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo mazuri katika michezo yao ya ligi wakianza na uliopo mbele yao dhidi ya Yanga.

# Simba SC yakatwa mtama, yaangukia Shirikisho Afrika

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Galaxy yavunja rekodi ya Wekundu hao Ligi ya Mabingwa kwa Mkapa huku...

HUKU ikikosa mabao mengi ya wazi, Mabingwa wa soka Tanzania Simba, jana walikatwa 'mtama' na kujikuta wakiangukia Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kukubali kipigo cha mabao 3-1 kwenye mechi ya marudiano dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Licha ya kushinda mabao 2-0 ugenini, nchini Botswana, Simba imetolewa kwenye michuano hiyo kwa bao la ugenini baada ya matokeo ya jumla ya mabao 3-3, lakini Jwaneng Galaxy imetinga hatua ya makundi, kwa faida ya mabao mengi ugenini.**

Mabingwa hao wa Tanzania sasa wanakwenda kucheza Kombe la Shirikisho Afrika na timu ambazo zimetinga kwenye raundi ya pili.

Kipigo hicho, kimemaliza rekodi nzuri ya Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo timu hiyo ilikuwa ni kama 'machinjioni' kwa wageni.

Mabao yote ya wageni yalifungwa kipindi cha pili, huku Simba ikitangulia kupata bao dakika ya 40 likifungwa na Rally Bwalya.

Waliopeleka msiba Msimbazi walikuwa ni Rudath Wendell aliyefunga mabao mawili na Gape Mohutsiwa.

Wendel alisawazisha bao sekunde chache tu baada ya kipindi cha pili, huku akifunga bao la pili dakika ya 59.

Yalikuwa ni makosa ya mabeki wa Simba kumsindikiza mchezaji huyo kwenye bao la kwanza, huku Paschal Wawa akishindwa kuruka kuupiga kichwa mpira wa kurushwa, uliomkuta mfungaji akauweka wavuni kirahisi.

Baada ya hapo, wachezaji wa Simba walianza kucheza kwa wasiwasi, huku wakipoteza muda na haikushangaza walipopachikwa bao la tatu, dakika tano kabla ya mechi kumalizika, lililowekwa wavuni kwa kichwa na Gape, baada ya Aishi Manula na mabeki wake kuukosa mpira wa krosi na kiungo huyo mkabaji kuukwamisha wavuni, akimaliza ndoto za Simba kutinga makundi.

Iliwachukua Simba dakika tano tu kumsalimia kipa wa Jwaneng Galaxy, Ezekiel Morake, baada ya Bwally kupiga shuti kali la mbali lililookolewa na kipa huyo ambaye jana alifanya kazi ya ziada kupunguza magoli kwa timu yake.

Shomari Kapombe, Bernard Morrison na Bwalya, walikosa mabao ndani ya dakika moja, baada ya kutokea kizaazaa kwenye dakika ya 26 katika lango la Watswana hao, lakini kila mmoja alipokuwa akipiga, kipa Morake alikaa imara kuokoa michomo hiyo.

Sadio Kanoute naye alimegewa pande na Thadeo Lwanga dakika ya 38, akiwa karibu na eneo la hatari, alipiga shuti kali, lakini kama kawaida kipa Morake aliruka juu na kupangua, ikawa kona ambayo haikuzaa matunda.

Kipindi cha kwanza, Jwaneng Galaxy haikufanya shambulio lolote la hatari, lakini walifunguka kipindi cha pili na kuwa hatari wanapolikaribia lango la Simba.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >